

MASHABIKI WAMJIA JUU KLOPP

UKURASA 22

**ADAIWA** kuua mke wake kisa nyama ya mbuzi

UKURASA 3

**MWANAFUNZI** aliyepotea siku 26 asimulia alivyoishi porini

UKURASA 7



**WAKILI** Mkuu wa Serikali aokoa mabilioni mashauri korti ndani na nje

UKURASA 7


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Ijumaa Oktoba 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581826

www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

0745 700 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital


# Wataka mbadala wa adhabu ya kifo

**WASEMA** ni mzigo kwa serikali, waliohukumiwa na kunusurika watoa shuhuda nzito...*Ukurasa wa 2*



UKURASA WA 8

## SERIKALI YATIMIZA MATAKWA 11 YA MKUTANO WA HABARI

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, amesema serikali imetimiza kwa kiwango...

UKURASA WA 24

## MKUDE: SIMBA, YANGA ZINAFANANA

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amebadili aina ya mazoezi katika kikosi chake kuelekea mechi ya watani wa...



# Askofu Malasusa atoa somo uchaguzi Serikali za Mitaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, amewapa somo wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu, akiwataka wasijisahaulishe kwamba



matendo yao yanapaswa kuwa yamenyooka kuanzia duniani hadi mbinguni.

Malasusa, alisema kuna idadi kubwa ya watu hawatambulishiki kwenye jamii hivi sasa, kwa sababu ya matendo yao, hata wake zao hawawezi kuwatambulisha.

Alikuwa akihubiri jana katika Usharika wa Uuwo-Mwika wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, wakati wa ibada ya maziko ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, Prof. John Shao (80).

Prof. Shao, alifariki dunia Oktoba 6, mwaka huu wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali

ENDELEA UK. 2

## Taarifa miradi yenye dosari mbio Mwenge kutua kwa Rais

UKURASA 3

MICHEZO KUFUZU AFCON 2025 KWETU NI DENI - STARS UK. 24 | KATUNI UK. 6

# Askofu Malasusa atoa somo uchaguzi Serikali za Mitaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, amewapa somo wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu, akiwataka wasijisahaulishe kwamba matendo yao yanapaswa kuwa yamenyooka kuanzia duniani hadi mbinguni.

Malasusa, alisema kuna idadi kubwa ya watu hawatambulishiki kwenye jamii hivi sasa, kwa sababu ya matendo yao, hata wake zao hawawezi kuwatambulisha.

Alikuwa akihubiri jana katika Usharika wa Uuwo-Mwika wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, wakati wa ibada ya maziko ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, Prof. John Shao (80).

Prof. Shao, alifariki dunia Oktoba 6, mwaka huu wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya KCMC.

"Kuna watu hawatambulishiki kwenye jamii kwa sababu ya matendo yao, hata wake zao hawawezi kuwatambulisha. Profesa Shao yeye alikuwa anatambulishika wakati wa uhai wake.

"Tunaenda kwenye uchaguzi na wagombea watajitangaza sana mambo yao, wasisahau wanatakiwa mambo yao yanyooke na wajitangaze mbinguni."

Katika maziko hayo, viongozi wengine walioongozana na Askofu Dk. Malasusa, ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Frederick Shoo na Askofu mstaafu wa Dayosisi ya Iringa, Dk. Owdenberg Mdegela.

Akisoma wasifu wa hayati Prof. Shao, mtoto wa marehemu, Kunda Shao, alisema baba yake (Prof. Shao), aligomea matibabu ya nje ya nchi, akiamini madaktari wa ndani yaani Tanzania wana uwezo wa kufanya matibabu hayo.

Alisema baba yake, alikuwa akiugua ugonjwa wa saratani ya tezi dume.

Mwakilishi wa Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, Mkurugenzi wa Mafunzo wa Wizara hiyo (MoH), Dk. Saitore Laizer, alisema serikali haitasahau mchango wa nguli huyo katika mifumo ya sekta ya afya nchini.

"Kanisa limepata pigo, lakini pia sekta ya afya katika eneo la tiba na mafunzo, tumepata pigo. Profesa Shao alikuwa ni mbuyu mkubwa, lakini ulikuwa unazaa matunda kila mwaka. Serikali na sekta ya afya, haitasahau mchango wake hasa eneo la microbiolojia na immuniolojia," alisema Dk. Saitore.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, Prof. Gilleard Masenga, alisema katika kuuenzi mchango wa Prof. Shao, Shirika la Msamaria Mwema (GSF), limepanga kulipa hadhi ya jina lake moja ya majengo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba cha Tumaini (KCMCo).

Taarifa ya kifo chake, ilitangazwa na Katibu Mtendaji wa Shirika la Msamaria Mwema (GSF) na Mkurugenzi Mtendaji wa KCMC, Prof. Gilleard Masenga.

Wakati wa uhai wake, Prof. Shao, aliwahi kuwa Katibu Mtendaji wa GSF, Makamu Mkuu wa Kwanza wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA).

Prof. Shao, alizaliwa mwaka 1944, alisomea shahada ya magonjwa ya vimelea mbalimbali pia amewahi kuwa mkufunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1978-1981, Mshauri wa wanafunzi UDSM, kuanzia 1981-1986, Profesa Mshiriki mwaka 1982-1990, na Profesa tangu 1986.

Tangu mwaka 1994 alikuwa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Umoja wa Madaktari Afrika na mwaka 1992, aliwahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Mabadiliko ya Sekta ya Afya Tanzania, Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania Mwaka 1990-1992.

Katika maisha yake ya kitaaluma, aliandika na kuchapisha machapisho 150 ya kitaifa na kimataifa na alikuwa na maono binafsi kama kuanzisha KCRI na KCMCO


TANGAZO

Tunauza Material ya kuchanganya kwenye Lami/Pavement [Topcel Cellulose Fiber]

Kwa mawasiliano zaidi:

Estim Construction Co. LTD

Plot No. 83 Mikocheni

Industrial Area

0746941831

0746941907




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Wataka mbadala adhabu ya kifo

**Na Salome Kitomari**

WADAU wa haki jinai wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuweka adhabu mbadala kwa kosa la mauaji badala ya kunyongwa hadi kufa kwa kuwa haijawahi kutekelezwa tangu serikali ya awamu ya tatu huku wafungwa wengi wakikaa magerezani wakizidi kuumia kisaikolojia.

Wakizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Adhabu ya Kifo Duniani yenye kaulimbuiu 'Adhabu ya Kifo Hailindi Mtu Yeyote: Iondolewe Sasa', walisema wafungwa hao ni mzigo kwa serikali kutokana na kutunzwa kwa fedha za Watanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema lengo la adhabu ni kurekebisha tabia ili mtu awe mfano kwa wengine lakini wengi wako gerezani kwa muda mrefu na hawajui hatima yao.

"Adhabu ya kifo haifanyi kazi yoyote kwa kuwa wanalishwa kwa gharama za serikali, hivyo ni mzigo kwa taifa, Adhabu hii haijawahi kutekelezwa mwaka 1994. Ni miaka 30 sasa. Kama imeshindikana kutekelezwa ni muhimu kukawa na mbadala," alisema.

Pia alisema hakuna ushahidi kwamba adhabu hiyo imepunguza uhalifu bali kumekuwa na makosa mengi na kwamba hivi karibuni nchini Iran, kuna adhabu ya kifo na hata mwizi wa simu anapata adhabu hiyo na kwamba wamenyonga zaidi ya 200 lakini bado matukio yapo.

Dk. Henga alisema wako waliohukumiwa kifo kimakosa na baada ya muda wanaachiwa baada ya kukata rufani huku wengine hawajui taratibu ili wapate msaada kisheria na kwamba mtu anaponyongwa hakuna namna yoyote inawezekana kumrejesha.

"Tanzania ni nchi ya demokrasia lakini kutokana na mizizi ya kikoloni ndiyo maana sheria hiyo imeendelea kuwapo. Kuna mikataba mingi tumeridhia ukiwamo Mkataba wa Haki za Binadamu na Kiraia ambao unatambua haki za kuishi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Women Aid and Criminal Justice (WACT), Elizabeth Majagi, alisema wanawake wengi waliowatembelea wenye umri wa miaka 18 wanasema wengi walidanganywa wakubali makosa kisha watasaidiwa kutoka mbele ya safari.

"Watu wanasota sana gerezani hata kesi haijasikilizwa kwa miaka mingi na hawafahamu hatima yao. Segerea wako watatu wamekaa miaka tisa, mmoja aliingia akiwa na miaka 19. Hawajui kesi zao na uelewa wa sheria ni mdogo na wanaotoa msaada wa sheria ni wachache," alisema.

Alisema Kampeni ya Msaada wa Kisheria na Mama Samia imefika kwenye magereza mengi na kutoa msaada kwa wafungwa wengi wenye uelewa mdogo kisheria na kwamba wafungwa wengi hawawezi kukata rufani na wanatumikia kifungo pasipo utekelezaji.

Mkurugenzi wa Tanzania Exprisoners Foundation (TEPF), Rose Male, alisema alishtakiwa kwa mauaji ya dereva wa bodaboda ambaye alimpigia simu kutumia usafiri wake halafu baadaye aliuawa. Kutokana na tuhuma hizo, alisota mahabusu kwa miaka minne na baadaye kuhukumiwa kifungo cha kunyongwa hadi kufa lakini alitumikia miaka miwili kisha akakata rufani.

"Wengi ni wazee kutokana na kukaa kwa muda mrefu kutokana na adhabu ya kifo kutotekelezwa. Wengi wanaishi kwa hofu kwa kuwa wanahisi watanyongwa wakati wowote, mlango ukifunguliwa mtu anawaza nimekuja kuchukuliwa kwa ajili ya kunyongwa," alisema.

Alisema mfungwa wa adhabu ya kifo haruhusiwi kutembelewa bila ruhusa ya mkuu wa wilaya na wengi hawajui huo utaratibu ili wamfikie ndugu yake jambo ambalo linawanyima haki ya kupata taarifa.

"Katika kazi hizi nilikutana na dada mmoja alihukumiwa mwaka 1999 lakini hajawahi kupata nakala ya hukumu yake na hana rekodi yoyote ya kesi yake hata hakumbuki mahakama aliyohukumiwa, jambo ambalo limemnyima haki ya msaada wa kisheria," alibainisha.

Male alisema mtu ana kesi ya mauaji anapewa wakili wa serikali ambaye wakati mwingine hafanyi kwa ubora kwa kuwa wanawaambiwa washtakiwa wakiri makosa kwa kuwa watatoka mbele ya safari.

Alisema wafungwa wanapokuwa gerezani huzalisha lakini wanapomaliza vifungo hupewa nauli tu, huku wengine wanaporudi wanakuta familia zimeparaganyika, hivyo hawana pa kuanzia.

"Tumefanya utafiti tumebaini asilimia 60 ya walioko gerezani ni wakosaji wa kujirudia. Maana yake mtu anakwenda uraiani anapokewa kwa unyanyapaa, mali zake zimepotea, familia imeparaganyika hana pa kuanzia. Kama wanazalisha wakiwa gerezani basi serikali iwe inawawekea kwenye akaunti zao fedha kidogo ili wanapomaliza kifungo wawe na kianzio cha maisha," alisema.

Mwakilishi wa Children Education Society Organization (CHESO), Utty Mwang'amba, alisema kuna unyanyapaa kwenye jamii kiasi cha wanaotoka gerezani kushindwa kuoa au kuolewa na wengine kupata matatizo ya afya ya akili.

"Leo kuna familia imenitafuta inasema inahama eneo wanaloishi kutokana na unyanyapaa wanaokutana nao. Wanaonyoshewa vidole sana, wanaambiwa usiolewe pale, usioe pale. Mwingine anatoka gerezani anakuta mwenza wake ameshaoa au kuolewa, hivyo anakosa pa kuishi. Lazima tuwaangalie hawa watu," alisema.

Kuhusu sababu za mauaji, wachangiaji hao walisema wengi walioko gerezani ni kwa sababu ya kulipiza kisasi, wivu wa kimapenzi, imani za kishirikiana kutaka kupata utajiri na msongo wa mawazo.

**SERIKALI YAJIBU**

Mwakilishi wa Wizara ya Katiba na Sheria, Wakili Emmanuel Mbega, alisema suala la mabadiliko ya sheria ni mchakato na kwamba serikali inaendelea kupokea maoni ya wananchi na ili sheria ibadilishwe lazima kuwe na utafiti wa kina.

Alisema ni wajibu wa wakili kutoa msaada wa kisheria na kwamba malalamiko ya kwanza wanawalazimisha watuhumiwa kukiri makosa watalifuatilia, ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

# Adaiwa kuua mke kisa nyama ya mbuzi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linamshikilia mwanamume (jina limehifadhiwa) mkazi wa mtaa wa Chitepo, Mazwi, Manispaa ya Sumbawanga, kwa tuhuma za kumpiga kisha kumkata na kisu mke wake, Hawa Suleiman (31) na kumsababishia kifo.

Chanzo cha mauaji hayo kinadaiwa ni wivu wa kimapenzi. Inadaiwa kuwa mume huyo alichukizwa na kitendo cha kukuta mke wake amepika nyama ya mbuzi wakati hakumwachia hela yoyote ya matumizi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Shadrack Masija, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa mtuhumiwa anashikiliwa katika Kituo cha Polisi mjini Sumbawanga na anatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote upelelezi wa awali utakapokamilika.

SACP Masija alisema Hawa alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruswa mjini hapa.

Kwa mujibu wa Kamanda Masija, tukio hilo lilitokea Oktoba 9, mwaka huu, majira ya saa 7:00 baada ya kuzuka ugomvi baina ya wanandoa hao ndipo mwanamume alipoanza kumpiga mke wake kwa kutumia kipande cha mti na kumkatakata sehemu mbalimbali za mwili wake kwa kutumia kisu.

Mmoja wa majirani wa wanandoa hao, Editha Kawia, kabla ya mauaji hayo, mtuhumiwa aliondoka nyumbani kwake na kumwacha mke wake na kwenda kwenye shughuli zake bila kumwachia hela yoyote ya matumizi.

Alisema majira ya mchana, mwanamume huyo alirejea nyumbani na kukuta mke wake amepika nyama ya mbuzi na alipomhoji alikopata fedha ya kununua nyama hiyo, hakutoa majibu yaliyomridhisha.

"Mtuhumiwa alichukua sufuria iliyokuwa na mboga hiyo na kwenda kumwaga nje ndipo alipotoa Sh. 2,500 na kumpa mke wake ili akanunue mboga nyingine ambayo wataitumia kama kitoweo kwa siku hiyo kisha akaondoka zake," alisema.

Kwa mujibu wa jirani huyo, baada ya muda, mwanamume huyo alirejea nyumbani akakuta mke wake amenunua dagaa na kupika hali iliyomkera na kudai kuwa hawezi kula dagaa na kutishia kumpiga. Ili kujiepusha na kipigo, alisema mwanamke huyo alikimbia na kuondoka nyumbani.

"Hawa alikaa huko alikokimbilia na akarudi nyumbani majira ya saa 6;30 usiku akamkuta mume wake nyumbani. Alipoingia ndani ndipo ugomvi ulipoanza na mwanamume huyo akaanza kumpiga mke wake akimtuhumu kuwa na tabia mbaya.

"Baada ya kumpiga muda mrefu jirani yake alikwenda kuwagongea ili awasuluhishe lakini mwanamume alimjia juu jirani huyo akidai kuwa hayamhusu na anaweza kumpiga hata pia, kauli iliyomsababishia hofu na kuamua kurudi ndani ya nyumba yake," alisema.

Jirani huyo alibainisha kuwa mwanamume aliendelea kumpiga Hawa kwa muda mrefu kisha akaacha. Alisema kulipokucha alikwenda kutoa taarifa kwa mwenyekiti wa mtaa ndipo walipofika nyumbani kwa mtuhumiwa, wakamchukua akiwa na majeraha na kumpeleka hospitalini kwa ajili ya matibabu.




Mwenyekiti wa Bodi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Stephen Wasira (katikati), akionyesha kitabu cha Maono ya Nyerere katika uongozi na maendeleo katika zama mpya za maendeleo ya kiviwanda, baada ya kukizindua, wakati wa Kongamano maalumu la tatu la Kitaaluma la Kumbukizi ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, chuoni hapo, Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila (kulia), Naibu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Richard Kangalawe (kushoto) na Makamu Mwenyekiti wa chuo hicho, Fatma Ramadhan. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taarifa miradi yenye dosari mbio za Mwenge kukabidhiwa kwa Rais

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, amesema taarifa ya miradi iliyobainika kuwa na dosari katika mbio za Mwenge wa Uhuru 2024, itakabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua zaidi.

Pia amesema katika maadhimisho ya wiki ya vijana kwa mwaka huu kutakuwa na makongamano kwa ajili ya vijana yanayolenga masuala mbalimbali ikiwamo elimu ya sera mpya ya maendeleo ya vijana toleo la 2024 na mafanikio ya miaka 60 ya Mwenge wa Uhuru.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho hayo, kilele cha mbio hizo sambamba na kumbukumbu ya miaka 25 ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere yatakayofanyika jijini Mwanza, Waziri Kikwete alisema kupitia mbio hizo, kumebainika kuwapo na dosari katika baadhi ya miradi ikiwamo kujengwa chini ya kiwango na kutokuwa na usimamizi mzuri.

"Taarifa ya miradi iliyotembelewa na Mwenge nitakabidhiwa kwa Rais Samia, siku ya kilele kwa hatua zaidi," alisema.

Alisema kwa mwaka huu elimu ya mbio hizo itatolewa ili kusaidia kuongeza uelewa kwa Watanzania ambao wanahisi kuziendeleza ni upotevu wa fedha.

"Kuna watu wanaona Mwenge huu ni kama tochi, kuna wengine wanatamani usiwapo. Tunataka kueleza kwa nini Mwenge wa Uhuru upo. Usiache mambo yakazungumzwa, inawezekana kuna watu hawajui umuhimu, hii ni kama wanavyosherehekea siku zao za kuzaliwa," alisema.

Kuhusu Wiki ya Vijana, Kikwete alisema itazinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, leo na inalenga kuwakutanisha vijana kujadili fursa na vikwazo vinavyowakabili katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alisema vijana watajengewa uwezo katika uongozi na kuhamasishwa kujitambua na kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali.

Ridhiwani alisema hadi sasa serikali imewezesha vikundi vya vijana zaidi ya Sh. bilioni 31. "Tunatarajia zaidi ya vijana 500 watafanya maandamano ya amani wakiwa wamebeba ujumbe mbalimbali na sisi serikali tutakuwapo kuchukua na kufanyia kazi," alisema.

Kuhusu Kumbukizi ya Miaka 25 ya Mwalimu Nyerere, alisema, ibada maalum ya kumuenzi itafanyika katika Kanisa Katoliki Nyakahoja, mkoani Mwanza.

PSSSF Public Service Social Security Fund

## NOTISI YA MWISHO KWA WADAIWA WA MALIPO YA VIWANJA

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), unawataarifu wateja wake wote walionunua viwanja kwenye miradi ya uuzaji wa viwanja na ambao bado hawajakamilisha malipo kwa mujibu wa mkataba wa mauziano, kuhakikisha wanalipa madeni yote kabla ya 31 Disemba 2024.

Tangazo hili linawahusu wateja walionunua viwanja katika miradi ya Kiseke – Mwanza, Ibadakuli – Shinyanga, Usule – Tabora, Ilembo – Katavi, Mitwero – Lindi, Muriet – Arusha, Mawelewele – Iringa na Lukobe – Morogoro, Kimbiji – Dar Es Salaam, Unyinga- Singida, Buhembe na Kyasha Mugezi- Kagera.
Aidha, tangazo hili linawahusu pia wateja wote ambao walinunua viwanja kutoka kwa uliokuwa Mfuko wa PSPF kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko PSSSF mwaka 2018.

Hii ni notisi ya mwisho ambapo mteja yeyote ambae atashindwa kukamilisha malipo ya deni lake ndani ya muda uliopangwa, mkataba wake utasitishwa na kiwanja husika kitauzwa kwa mwombaji mwingine bila notisi nyingine ya ziada na bila kurejeshewa malipo ya awali.

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia nambari 0800 110 040 (BURE) au fika kwenye Ofisi zetu za Makao Makuu zilizopo PSSSF House Makole Road Dodoma ghorofa ya tatu (3) au kwenye ofisi zetu zilizopo karibu nawe.

**IMETOLEWA NA:**

**MENEJA MAHUSIANO NA ELIMU KWA WANACHAMA**

Leo.Kesho.Pamoja. www.psssf.go.tz 0800110040 psssftz

# HABARI PICHANI



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Letshego Faidika, Baraka Munisi (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Biashara, Asupya Bussi Nalingigwa (wa pili kulia), wakizungumza na mmoja wa wateja wa benki hiyo, walipotembelea moja ya matawi yao, jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi Mtendaji wa United Bank for Africa, Gbenga Makinde (katikati), akiwa na maofisa wa ukaguzi wa benki hiyo, Neema Mtutwa (kushoto) na Ketta Malaba katika maadhimisho ya Huduma kwa Wateja.



Wafanyakazi wa Ecobank Tanzania, wakiwa katika picha ya pamoja katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja.



Abdalla M. Mussa akipokea zawadi kwa niaba ya Gapco kutoka kwa Mkurugenzi wa Biashara PBZ Bank Ltd, Eddie Mhina katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya simu ya Tigo, Jerome Albou (kulia), akikabidhi zawadi kwa mmoja wa wateja katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja ambayo waliisherehekea kwa safari maalum kwa kutumia treni ya mwendokasi (SGR), ikiwa ni pamoja na maadhimisho ya kampuni hiyo, kutimiza miaka 30.



Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Diamond Trust Tanzania PLC, wakiwa katika picha ya pamoja ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja.

# Wakala ukusanyaji mapato jela miaka 20 ufujaji fedha za umma

**Na Vitus Audax,**

ALIYEKUWA wakala wa ukusanyaji mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza, Fred Chamata, amehukumiwa kifungo cha miaka 20 jela baada ya kukutwa na hatia ya ufujaji na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi katika Mahakama ya Wilaya ya Ukerewe na Hakimu Mkazi Mkuu Lucas Nyahenga.

Makosa hayo ambayo Chamata alikuwa anakabiliwa nayo ni kinyume cha vifungu vya 28 (1) na 31 vikisomwa pamoja na Aya ya 21, jedwali la kwanza vyote vya Sheria namba 326 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza, Moses Malewo, alidai pia makosa hayo ni kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumu Sura ya 200 kifungu cha 57(1) na 60(2) na (3), ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022. Alidai mshtakiwa alifikishwa mahakamani hapo katika kesi ya Uhujumu Uchumi Na. 06/2023 kwa madai ya kushindwa kuwasilisha Sh. 16,245,550 katika akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe.

Malewo alidai fedha hizo alizikusanya kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato vya halmashauri hiyo akiwa wakala wa kukusanya mapato.

Alidai kuwa mshtakiwa alifanya hivyo akijua ni kinyume na Memoranda ya Fedha za Halmashauri za Mwaka 2009 lakini pia Kinyume cha Sheria ya Fedha za Halmashauri Sura ya 290 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Alidai sheria hizo zote zilimtaka kila alipokusanya mapato, kuyawasilisha kwenye akaunti za halmashauri kila siku anayokusanya au kesho yake endapo kuna changamoto.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Nyahenga alisema sambamba na kifungo cha miaka 20 jela, anatakiwa pia kurejesha katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe Sh. 16,245,550.



Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. John Rwegasha (katikati), akikata utepe kuzindua maonesho 25 ya kimataifa 2024 ya vifaa tiba, katika ukumbi wa Diamond Jubilee, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika wa Expo, Dancan Njage. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TPA yajipanga kupanua bandari kuboresha huduma

**Na Joseph Mwendapole**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, amesema mamlaka hiyo imejipanga kufanya upanuzi wa bandari zake ili kuendelea kutoa huduma shindani katika soko la Afrika na kimataifa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja, Mbossa alisema mpaka sasa TPA imejiweka katika nafasi nzuri zaidi ya kiushindani kutokana na uwekezaji wake unaoendelea katika bandari mbalimbali hapa nchini.

Mbossa alisema mamlaka ina nia ya kupanua na kujenga gati 10 katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi na tija katika bandari hiyo.

"Katika kuhakikisha wateja wetu wanaendelea kupata huduma bora na stahiki sisi kama mamlaka tumekuja na mpango wa kuongeza gati 10 katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Hii inaenda kupanua soko la biashara kwa watumiaji wa bandari yetu kwani ufanisi utakuwa ni mkubwa na utakidhi mahitaji ya wateja wetu", alisema. Mbossa pia alisema TPA imeendelea kuboresha miundombinu ya bandari zake ambazo ni pamoja na Bandari ya Bagamoyo, Bandari ya Tanga, Mtwara, Mbamba Bay na bandari zingine ambazo ziko chini ya mamlaka hiyo.

Alisema hayo yote yanafanyika ili kuhakikisha kuwa TPA inachochea uchumi wa Taifa kupitia bandari zake kwa kushirikiana na wawekezaji waliopo.

"TPA tumejipanga kuufungua uchumi wa Taifa kwa kutumia bandari zetu na ndio maana tumeendelea kuboresha maeneo mengi ya bandari zetu ili ziweze kutoa huduma kwa wateja wetu wa ndani na nje ya nchi.

"Kupitia uwekezaji ambao tumeufanya katika bandari zetu, matunda yake tumeanza kuyaona ambapo hadi sasa kumekuwa na utofauti mkubwa katika huduma za bandari ukilinganisha na miaka kadhaa ya nyuma.

"Hii inatokana na juhudi za serikali katika kuleta mageuzi makubwa ya kiutendaji katika bandari zetu ili kuchochea biashara zaidi na kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema.

Mbossa alisema hadi kufikia sasa, sekta ya uchukuzi inachangia zaidi ya asilimia 7.3 ya pato la taifa ikiwa malengo yaliyopo ni kufikisha asilimia 15 . "Ili kufikia malengo, TPA tumeanza kuungana na makampuni makubwa ya meli duniani ili kuhakikisha bidhaa zinakuja kwa wingi na kwa bei rahisi ili kuwarahisishia na kutanua wigo wa kibiashara na mataifa ya jirani. "Pamoja na maboresho ya bandari zetu, TPA imeendelea kuboresha mifumo ya malipo hasa katika mfumo wa kidijitali ambayo itamwezesha mteja kulipia bidhaa au mzigo wake popote alipo badala ya kwenda ofisini, alisema.

Mbossa aliwataka wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kuendelea kutumia bandari za Tanzania katika kusafirisha mizigo yao kwani ufanisi uliopo kwa sasa katika bandari hizo ni mkubwa kulinganisha na awali.

Naye Mkuu wa Uendeshaji wa Kampuni ya Tanzania East Africa Getway Terminal Limited (TEAGTL), Donald Tawala, alisema bandari imekuwa ikiboresha huduma zake katika maeneo tofauti tofauti, hivyo wao kwa kushirikiana na TPA wameendelea kufanya mageuzi makubwa katika uboreshaji wa huduma wanazozitoa.

Alitaja baadhi kuwa ni pamoja na uboreshaji wa mifumo ya malipo, uboreshaji wa mifumo ya kupakia na kushusha mizigo katika meli na lengo mageuzi hayo ni kuhakikisha ufanisi katika bandari unaongezeka na kuwa na tija.

# Waziri Kombo ahimiza ushirikiano wa kibiashara

**Na Halfani Chusi**

TANZANIA imesisitiza umuhimu wa kukuza ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji na nchi marafiki, ikiamini kuwa hiyo ndiyo njia bora zaidi ya kukuza uchumi kwa manufaa ya wananchi.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo, alisema hayo jana Helsinki, Finland, aliposhiriki kikao cha Mashauriano ya Kisiasa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Finland, Elina Valtonen na Naibu Mawaziri wa Wizara hiyo, Pasi Hellman anayeshughulikia masuala ya Maendeleo ya Kimataifa na Jarno Syrjälä anayeshughulikia biashara za kimataifa. Kombo alisema Tanzania imefanya mabadiliko makubwa ya mifumo ya sera na sheria ili kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kuvutia uwekezaji.

Kupitia hali hiyo, alitoa wito kwa wawekezaji wenye mitaji na dhamira ya dhati ya kuwekeza, waondoe hofu kuhusu Tanzania kwa kuwa ni mahali salama kwa wawekezaji na mitaji yao.

Waziri Kombo aliishukuru serikali ya Finland kwa kufanya juhudi kubwa ya kuisaidia Tanzania katika maeneo mbalimbali kama vile misitu, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), mifumo ya ulipaji kodi, hali ya hewa na elimu. Alisema juhudi hizo zimechangia kuifikisha Tanzania ilipo sasa na kuwaomba mawaziri hao waendeleze juhudi hizo huku wakihimiza kampuni za nchi yao kuwekeza Tanzania ambayo ina fursa nyingi ambazo hazijatumiwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo mitaji midogo na teknolojia duni.

Balozi Kombo aliainisha maeneo ambayo Finland inapaswa kuwapa kipaumbele katika ushirikiano wake na Tanzania kuwa ni pamoja na uhawilishaji wa teknolojia, nishati, viwanda vya kuongoza thamani, elimu ya ufundi, masuala ya kijinsia na haki za wanawake na masuala ya kidijiti.

Alisema maeneo hayo yakifanyiwa kazi ipasavyo, yataongeza nafasi za kazi na ni suluhisho la moja kwa moja la tatizo la ajira nchini.

Kombo aliongeza ni wakati mwafaka wa nchi ya Finland kutoa ufadhili wa masomo kwa vijana wa Tanzania katika fani ambazo nchi hiyo pia inazihitaji kwa kiasi kikubwa. Alisema Tanzania iko tayari kutuma vijana ambao watasomeshwa kwa viwango vinavyohitajika katika fani hizo ili kuziba pengo kama vile la wataalamu wa afya hasa wauguzi katika nchi za Ulaya.

Viongozi hao pia walijadili suala la amani na usalama duniani na kusisitiza umuhimu wa kutatua migogoro inayoendelea kwa njia za kidiplomasia.

Waziri Kombo aliwahakikishia viongozi hao kuwa Tanzania itaendelea kuwa mstari wa mbele katika suala la kulinda amani na kwamba hivi sasa, Rais Samia ni Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ufungaji wa mita za maji kabla kutumia uharakishwe

**HUDUMA** ya majisafi na salama imekuwa na kero mbalimbali zikiwamo upungufu kwa sababu ya ukame au kuharibiwa kwa vyanzo vya maji. Sababu nyingine ni uharibifu wa miundombinu unaotokana na uhujumu au kupasuka mabomba.

Pia kumekuwa na urasimu wa watu kuunganishiwa huduma licha ya kulipia gharama zinazotakiwa. Aidha, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wateja ya kubambikiwa bili za maji au kutozwa bili zile zile hata kama hawapati maji.

Malalamiko mengi kuhusu huduma za maji, yako katika maeneo ya mijini hususani miji mikubwa kama Dar es Salaam. Hivi sasa kwa mfano, wateja wanaotegemea huduma hiyo kutoka Ruvu Juu, wako katika adha kutokana na upungufu wa maji, hali inayowafanya wapate kwa mgawo. Yako baadhi ya maeneo ambayo wananchi wanalalamika kuwa hawajapata maji kwa zaidi ya wiki moja.

Ni jambo la faraja kwamba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ambayo pia inahudumia baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani, imekiri kuwapo na upungufu huo na kuwaahidi wateja wake kuwa inalifanyia kazi suala hilo.

Kuwapo kwa upungufu au changamoto katika huduma hiyo, serikali imekuwa ikifanya kila juhudi kuhakikisha wananchi wanaondokana na adha hiyo ili kutumia muda mwingi kufanya kazi za uzalishaji badala ya kusaka maji. Kupitia mpango huo, pia kumekuwa na kampeni ya Rais Samia Suluhu Hassan iitwayo 'kumtua mama ndoo kichwani'.

Aidha, katika kutatua baadhi ya kero kama vile malalamiko ya wateja kubambikiwa bili au kutozwa bili zile zile hata kama maji hayapatikani, serikali imebuni mbinu ya kufunga mita za kulipia kabla ya kutumia (prepaid). Mfumo huu, kwa mujibu wa serikali, utakuwa mwarobaini dhidi ya malalamiko ya wateja. Kama ilivyo kwa umeme kupitia Lipa Umeme Kadiri Unavyotumia (LUKU), baada ya kufungwa kwa mita hizo hakutakuwa na malalamiko tena ya kubambikiwa bili kwa sababu mtumiaji atapata maji kutokana na fedha alizolipia.

Katika baadhi ya mikoa mita hizo zimeshafungwa na mkoani Dar es Salaam, mchakato wa kutekeleza suala hilo unaendelea. Kuwapo kwa mita hizo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuondosha baadhi ya kero kwa wateja kwa kuwa katika mikoa iliyoanza kutumika kwazo, kumekuwa na matokeo chanya.

Kwa jumla, mfumo wa kulipia maji ni mzuri na unapaswa kuharakishwa kwa sababu mbalimbali na kupunguza malalamiko na madai ya wateja kubambikiwa bili, una manufaa makubwa.

Miongoni mwa mafanikio hayo ni gharama za uendeshaji za mamlaka za maji zikiwamo kuwa na wafanyakazi wanaopita mitaani kusoma mita za maji. Gharama za kuajiri watu kwa ajili ya kusoma mita zitaokolewa na kutumika katika kuongeza tija na ufanisi kwa mamlaka husika.

Mfumo huo pia utaziwezesha mamlaka za maji kupata faida zaidi kutokana na makusanyo yanayotokana na kulipia huduma kabla ya kutumia tofauti na ilivyo sasa. Kwa mfumo uliopo sasa ambao mamlaka zimekuwa zikufuatilia madeni ambayo ni zaidi ya mabilioni ya shilingi, zimejikuta zikishindwa kujiendesha kikamilifu ikiwamo kupanua wigo wa huduma.

Mfumo mpya wa mita ya kulipia huduma kabla, utaziwezesha mamlaka kufanya maendeleo makubwa zaidi kwa kuwa zitakuwa zinapokea fedha bila shida kwa kuwa hakutakuwa na madai baada ya kutumia maji. Mteja atakuwa anatumia maji kwa kiasi cha fedha alicholipia. Hatua hiyo pia itaongeza nidhamu ya hali ya juu kwa mteja kwa kuwa hatakuwa radhi kuacha mabomba wazi na kumwaga maji kama ilivyo sasa. Ni wazi kwamba kwa kawaida, binadamu siku zote ni mgumu kukubali mabadiliko na ujio wa mita za maji za kulipia kabla, utapata upinzani kutoka kwa baadhi ya wateja kama ilivyokuwa LUKU. Kwa kuwa ni mfumo wenye manufaa, hauna budi kutekelezwa ili kuziwezesha mamlaka kuepuka madeni na kulinda maji.

Wahenga wanasema kawia ufike. Mita za kulipia kabla ya kutumia maji zimechelewa lakini zimekuja kwa watati mwafaka. Mchakato wa kuzifunga uharakishwe ili kuleta tija katika huduma ya maji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Robo karne baada ya kifo cha Mwalimu Nyerere, aliyoyafanya yasisahaulike



Na Adam Fungamwango

**JUMATATU** ijayo, Tanzania itaadhimisha miaka 25 ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano, Julius Kambarage Nyerere, aliyeondoka juu ya uso wa dunia, Oktoba 14, 1999. Ni siku ya kitaifa.

Alifariki dunia nchini Uingereza kwenye Hospitali ya Mtakatifu Thomas, jijini London, ambako alikwenda kwa matibabu ya kansa ya damu.

Nyerere alipenda zaidi kuitwa Mwalimu, kuliko vyeo vingine vyote alivyokuwa navyo, licha ya kwamba jina lake kuwa kubwa si Afrika tu bali duniani, lakini aliishi maisha ya kawaida kabisa na mwenyewe alipenda kulima kwa kutumia mkono.

Alikuwa mmoja wa viongozi wanaoheshimika zaidi barani Afrika na kuna wakati alikuwa Mwenyekiti wa Nchi Tano zilizo Mstari wa Mbele Kwenye Ukombozi wa Bara la Afrika.

Hiyo ilitokana na baadhi ya nchi wakati huo zilikuwa hazijapata uhuru na mwenyewe alisisitiza kuwa, Tanzania haiwezi kuwa huru, kama Afrika yote haitokuwa huru, jambo ambalo limeleta matunda, kwani hadi leo hakuna nchi ambayo haijapata uhuru.

Kwa bahati nzuri alifariki akishuhudia nchi zote zilifanikiwa kuwaondoa wakoloni. Wengi watamweleza kwa makubwa kama hayo aliyoyafanya, Afrika na dunia kwa ujumla, kwani alionekana kama si raia wa Tanzania pekee, bali alitegemewa na nchi nyingi kwa ushauri, busara na maono yake.

Binafsi nitamwelezea kwa vitu vidogo vya kawaida sana hasa kwenye maisha halisi ya Mtanzania, ambayo ameyafanya kipindi akiwa madarakani.

Kwanza kabisa, shule zilikuwa bure kabisa, kiasi kwamba hata madaftari, kalamu na vitabu vya masomo vilipatikana shuleni. Mwanafunzi anapomaliza na mwalimu kusaini anakwenda ofisini kupewa kingine.

Pamoja na ukweli hakukuwapo teknolojia kubwa kama sasa na kuna wakati uchumi wa chini, lakini ni kipindi ambacho wananchi walitibiwa bure kabisa hospitalini.

Hata chakula kilikuwa kinapatikana bure, hakukuwapo ulazima wa ndugu yoyote kupeleka chakula hospitalini. Wagonjwa wa kifua kikuu walilazimika kubaki hospitalini wakiwa wamelazwa mpaka itakapohakikishwa kuwa virusi ya ugonjwa huo vimedhohofika na hawezi tena kumwambukiza mtu mwingine. Kulikuwa na mabomba ya bure, kinamama wakitoka majumbani kwao kwenda kuchota na yakawa maarufu kama mabomba ya bure.

Cha ajabu mengine yaliwekwa hadi maeneo ambayo hayakuwa na watu wengi kama vile Sinza, Dar es Salaam wakati huo, kukiwa na pori na mashamba ya mpunga.

Kumbe ilishapigwa mahesabu kuwa baada ya miaka 10 na zaidi watakuja kuishi watu, kweli ikawa hivyo. Leo 'Sinza ni Jiji' la Dar es Salaam. Palikuwapo malori yanayojulikana kwa sasa kama maboza, yanazunguka mitaani ili wananchi wachote maji.

Watachota tani zao bila ya malipo hadi waridhike ndipo yanapoondoka. Maeneo ya Gezaulole, Kibugumo, Mwanadilatu, Kunduchi, Bunju, Boko, Kibada watu walipewa maeneo bure, tena kwa kulazimishwa, kipindi cha utawala wake.

Ilikuwa ni operesheni ya kupunguza watu wasio na kazi na ajira ya kueleweka jijini Dar es Salaam. Walikamatwa na kupelekwa sehemu hizo ambazo wakati huo zilikuwa mapori. Wengine walitoroka. Waliobaki, wao wenyewe au vizazi vyao vinakula matunda yake. Ni sehemu ambazo kwa sasa zina huduma zote muhimu, na ardhi imekuwa ghali sana. Hizo zilikuwa ni sera zake.

Mwacheni tu mzee wa watu alale mahali pema peponi, kwani amefanya mema kwa wananchi wake, ndiyo maana alipofariki wengi walilia sana. Wengine hawakuamini mtu kama Nyerere anaweza kufa mapema kiasi kile, ingawa alishafikika umri wa miaka 77. Huko nyuma awali alishahubiri upeo wa umri wake, kwa kurejea Maandiko Matakatifu kwamba, "Mtu ataishi umri wa makumi mawili matatu na kumi moja... (miaka 70)."

## HABARI KITAIFA

# Mwanafunzi aliyepotea asimulia alivyoishi porini

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MWANAFUNZI wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Bagara, Babati mkoani Manyara, Joel Mariki, amepatikana baada ya kupotea kwa siku 26.

Mariki (14) ambaye alipotea baada ya kuachwa na wanafunzi wenzake walipokuwa Mlima Kwaraa, amesema siku zote hizo alikuwa anaishi kwa kula majani na matunda pori.

Mwanafunzi huyo alipotea Septemba 14, mwaka huu, akiwa na wenzake kwenye ziara ya kimasomo katika Mlima baada ya kuachwa na kubaki porini.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magari, jana alithibitisha kumpokea mtoto huyo baada ya kupatikana.

Dk. Magari alisema hali yake si mbaya lakini wanaendelea kumfanyia uchunguzi.

Alisema afya yake itaendelea kuimarika akiwa anapatiwa matibabu hospitalini hapo.

Mama wa mwanafunzi huyo, Germana Wilbard, alikiri kupokea simu ambayo ilikuwa ikimwarifu kupatikana kwa mtoto wake.

Alisema mtoto wake alipotoka porini, aliibukia kwa mtu na kumweleza kuwa ana njaa ndipo alimpatia uji na akakumbuka namba za simu zake (mama) na kuomba ampigie, alipewa kisha akampigia.

> **Alisema mtoto wake alipotoka porini, aliibukia kwa mtu na kumweleza kuwa ana njaa ndipo alimpatia uji na akakumbuka namba za simu zake (mama) na kuomba ampigie...**

Alikiri kuwa mtoto wake anaendelea vizuri na anapata matibabu Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara japo amedhoofika.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Makarani Ahmed, akizungumzia tukio hilo kwa njia ya simu, alikiri kuwa ni kweli mtoto huyo amepatikana.

Ahmed alisema mtoto huyo yuko hospitalini kwa sasa na leo watakwenda kumfanyia mahojiano huko hospitalini.

"Jitihada za polisi kumtafuta zilikuwa kubwa mpaka tulirusha dron ili kumtafuta,"alisema Ahmed.

Alisema kwa taarifa ambazo si rasmi, mwanafunzi huyo alijitenga pembeni kwenda kujisaidia na aliporudi hakuwakuta wenzake, hivyo ameishi porini kwa kula matunda pori akiwatafuta wenzake.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Ahmed aliwataka walimu kuchukua tahadhari wanaposafiri na wanafunzi kwa kuwa walivyokuwa wanaulizwa ushahidi wa idadi ya wanafunzi waliokwenda nao Mlima Kwaraa, hawakuwa na majibu ya kuridhisha.

Pia alisema mtoto huyo alidaiwa kuwa mtukutu, hivyo alisisitiza walimu kutokukubali kubeba wanafunzi wa aina hiyo ili kuepuka usumbufu.

# Wakili Mkuu wa Serikali aokoa mabilioni mashauri mahakamani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeokoa zaidi ya Sh. bilioni 602 kipindi cha mwaka 2023/24 katika mashauri ya madai yaliyokuwa yamefunguliwa kwenye mahakama za ndani na nje ya nchi.

Pia, imeokoa Dola za Marekani milioni 817.6 na Euro milioni mbili katika mashauri hayo kwa njia ya usuluhishi.

Akifungua mkutano wa Baraza la Pili la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo jana kwa mwaka 2024/25, Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye ni Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Ally Possi, alifafanua kuwa kwa kipindi hicho Ofisi imesajili na kuendesha mashauri ya madai 9,650 kati yake 9,519 ni ya kitaifa (zaidi ya asilimia 60 ya mashauri yakiwa ni

migogoro ya ardhi na mashauri 131 ni ya kimataifa.

"Katika kuendesha mashauri hayo, 1,412 yalimalizika na ofisi imeokoa Sh. bilioni 536.51 na pia ofisi imeshughulikia mashauri ya usuluhishi 201 ambapo, kati yake 170 ni ya usuluhishi wa ndani na mashauri 31 ni ya usuluhishi wa kimataifa."

"Kati ya mashauri 201 yaliyoshughulikiwa, mashauri 43 yamemalizika kwa njia ya majadiliano, mahakamani na kwenye mabaraza ya usuluhishi. Kumalizika kwa mashauri haya, ofisi imeokoa Sh. bilioni 66.02, Dola za

Marekani 817,643,693.12 na Euro milioni mbili," alisema.

Kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa, alisema ni muhimu katika jamii na utawala kwa kuwa ndio kiungo muhimu katika kuhakikisha serikali inaweka miundombinu chanya ya huduma za kijamii kwa kuzingatia uwiano sawa na wananchi walioko katika eneo husika."

Alisema ofisi hiyo itakuwa na jukumu la kusimamia kesi zitakazotokana na uchaguzi na kuwahimiza kufanya kazi hiyo kwa weledi.

"Naomba hadhira hii kujiandikisha na kutumia nafasi na fursa hii ya kikatiba kuchagua viongozi sahihi kwenye mitaa yetu watakaosaidia kutuletea maendeleo kwa wakati," alisema.

Awali, Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Alice Mtulo, aliwataka wafanyakazi wa ofisi hiyo kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi.

Alisema kati ya Julai 2023 hadi Juni 2024, watumishi 80 wamepata mafunzo ndani na nje ya nchi, pamoja na kuboresha ofisi kwa kuweka vifaa 69 vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ofisi za mikoa na makao makuu.


**halotel**

**TAARIFA KWA UMMA**

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano inayoendelea kuboresha huduma na kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga simu na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama zetu za makato pindi mteja atakapokuwa hajajiunga kwenye kifurushi.

**GHARAMA ZA NDANI YA NCHI**

| Kipengele | Gharama |
|---|---|
| Kupiga Halotel kwenda Halotel | 10 Tsh/Dk |
| Kupiga Halotel kwenda mitandao mingine | 20 Tsh/Dk |
| Kutuma SMS | 5 Tsh/SMS |
| Data (MB) | 9.35 Tsh/MB |

**GHARAMA ZA NJE YA NCHI**

GHARAMA ZA KUPIGA SIMU NJE YA NCHI

| Kanda | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| **Ukanda 1:** USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| **Ukanda 2:** Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| **Ukanda 3:** Rwanda, Afrika Kusini, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| **Ukanda 4:** Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| **Ukanda 5:** Burundi | 1,350 |
| **Ukanda 6:** Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| **Ukanda 7:** Mitandao ya satelite | 13,800 |

GHARAMA ZA KUTUMA SMS NJE YA NCHI

| SMS | Gharama |
|---|---|
| SMS kwenda nje ya nchi | 95 Tsh/SMS |

| Aina ya kifurushi | Muda | Gharama (Tsh) | Mitadao Yote (Dk) | Halotel-Halotel (Dk) | SMS | Data (MB) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **VIFURUSHI VYA SAUTI** | | | | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 350 | 25 | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | | 110 | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | 60 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku | 1,000 | 180 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku 2 | 1,000 | 160 | | 25 | |
| Dakika & SMS | Siku 5 | 1,000 | 130 | 150 | 500 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 1,500 | 180 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 2,500 | 350 | 50 | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 3,000 | 500 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 4,000 | 400 | 50 | 50 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 5,000 | 550 | 650 | 100 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 10,000 | 1,600 | 1,600 | 150 | |
| Dakika & SMS | Bila Kikomo | 500 | 20 | | | |
| **VIFURUSHI VYA SMS** | | | | | | |
| SMS | Siku | 100 | | | 200 | |
| SMS | Wiki | 500 | | | 2000 | |
| SMS | Mwezi | 1,000 | | | 10,000 | |
| **VIFURUSHI VYA INTANETI** | | | | | | |
| Intaneti | Siku | 350 | | | | 170 |
| Intaneti | Siku | 500 | | | | 246 |
| Intaneti | Siku | 1,000 | | | | 492 |
| Intaneti | Siku | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Siku 10 | 2,100 | | | | 1,024 |
| Intaneti | Wiki | 1,000 | | | | 492 |
| Intaneti | Wiki | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Wiki | 3,000 | | | | 1,475 |
| Intaneti | Wiki | 5,000 | | | | 2,460 |
| Intaneti | Wiki | 10,000 | | | | 4,925 |
| Intaneti | Mwezi | 10,000 | | | | 4,920 |
| Intaneti | Mwezi | 20,000 | | | | 9,850 |
| Intaneti | Mwezi | 30,000 | | | | 14,780 |
| Intaneti | Miezi 2 | 50,000 | | | | 24,600 |
| Intaneti | Bila Kikomo | 500 | | | | 200 |
| **VIFURUSHI VYA COMBO** | | | | | | |
| Combo | Siku | 500 | 15 | 10 | 5 | 200 |
| Combo | Siku | 1,000 | 60 | | 60 | 246 |
| Combo | Wiki | 2,000 | 55 | | 20 | 850 |
| Combo | Wiki | 2,500 | 20 | | 20 | 1,150 |
| Combo | Wiki | 3,000 | 100 | | 30 | 1,250 |
| Combo | Siku 10 | 3,100 | 150 | 20 | 300 | 1,024 |
| Combo | Mwezi | 10,000 | 280 | | 50 | 4,000 |
| Combo | Mwezi | 20,000 | 400 | | 100 | 8,500 |
| Combo | Mwezi | 50,000 | 600 | | 200 | 22,000 |

# Adaiwa kuuawa kisa deni la kuku

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKAZI wa kijiji cha Leguruki, wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Israel Paulo (36), amefariki dunia kwa madai ya deni ya Sh. 15,000 lililotokana na mauzo ya kuku wa jirani.

Kabla ya kupoteza uhai, Paulo anadaiwa kupitia mateso makali, ikiwamo kupondwa pondwa korodani na uume na watu wawili wanaodaiwa kutekeleza unyama huo kwa kisingizio cha kutolipwa fedha za mauzo ya kuku wao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Justine Masejo, alithibitisha kwamba Paulo alifariki dunia Oktoba 5, mwaka huu, wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Arumeru (Tengeru), baada ya kujeruhuhiwa sehemu mbalimbali za mwili na watuhumiwa hao.

Kwa mujibu wa Kamanda Masejo, mpaka kufikia sasa polisi imewatia mbaroni watuhumiwa wawili wa mauaji hayo ambao ni ndugu wa familia moja.

Aliwataja wanaoshikiliwa kwa tuhuma za mauaji hayo kuwa ni Ndewario Lazaro (60) maarufu 'Shombotoni' na mwanawe, Oscar Ndewario (29).

Shombotoni ni mkazi wa kijiji cha Maruvango, Arumeru wakati Oscar ni mkazi wa Moivaro katika Halmashauri ya Jiji la Arusha na alikamatwa akitoroka kwenda kujificha Simanjiro, mkoani Manyara.

"Watuhumiwa wote wawili tunawashikilia kwa mahojiano zaidi. Upelelezi wa tukio hilo bado unaendelea na ukikamilika, jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria," alisema Masejo.

Alisema mwili wa Paulo umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Tengeru, ukisubiri taratibu za maziko.

Akizungumza kwa sharti la kutotajwa jina lake, mkazi wa kijiji cha Leguruki ambaye ni jirani na familia ya marehemu, alisema Paulo alishambuliwa na watuhumiwa hao kutokana na madai ya kutowapa fedha za kuku aliyepewa akauze.

"Marehemu amekufa kifo kichungu cha maumivu makali kwa sababu amefanyiwa ukatili mbaya wa kupigwa lakini pia kuharibiwa sehemu zake za siri na sehemu ya haja kubwa," alisema.

Pia alisema walikuwa wanaendelea na taratibu za mazishi na kwamba familia ilipanga ndugu yao kuzikwa jana nyumbani kwao, Lenguruki.



Mhitimu wa Shahada ya Awali ya Biashara katika Taaluma ya Benki na Huduma za Kifedha, Zulfa Badru (katikati), akipongezwa na mama yake mzazi, Jacqueline Amlungi, baada ya kutunukiwa katika Mahafali ya 54 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam juzi. Kushoto ni baba yake, Badru Iddi. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali yatimiza matakwa 11 ya mkutano wa habari

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, amesema serikali imetimiza kwa kiwango kikubwa maeneo 11 yaliyopitishwa katika Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya Habari (WSIS) uliofanyika miaka 20 iliyopita.

WSIS ni mfululizo wa mikutano inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa (UN), ikiwa na lengo la kujadiliana kuhusu fursa na changamoto zinazoletwa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika karne hii ya sasa.

Waziri Silaa aliyasema hayo jana wakati akifungua kikao kazi cha siku tatu ambacho kimejikita kufanya mapitio katika maeneo 11 ambayo nchi za Afrika zimejiwekea awali katika mkutano wa WSIS.

Kikao hicho kimeandaliwa na serikali kwa kushirikiana na Kamisheni ya UN kuhusu Uchumi wa Afrika (ECA) na kuwaleta pamoja watunga sera, wataalamu na wadau kutoka Afrika na nje ya bara hilo.

Wamekutana kufanya tathmini na upungufu katika utekelezaji wa mikakati waliyojiwekea katika miongo miwili iliyopita na kuimarisha ushirikiano wa kujenga jamii ya kidijitali shirikishi na endelevu.

Kupitia kikao hicho wadau hao watafanya mapitio kuona maeneo 11 ambayo nchi za Afrika zilijiwekea yamefikia wapi, wana changamoto gani na yapi ya kujifunza kwa ajili ya kuelekea mkutano wa mwakani.

Waziri Silaa aliyaanisha maeneo hayo kuwa ni pamoja na upatikanaji wa maarifa kwa wote kuanzia ngazi ya taifa hadi kimataifa.

"Kuhimiza na kuimarisha ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi na jamii ili kufikia mawasiliano jumuishi na endelevu.

Kadhalika, walikubaliana kuhusu kuendeleza miundombinu ya TEHAMA ili kuhakikisha hakuna kundi linaloachwa nyuma.

Pia walikubaliana umuhimu wa kujenga ujuzi na uwezo wa kutumia TEHAMA, kuimarisha usalama wa mtandao na ulinzi wa taarifa binafsi, Waziri Silaa alisema, Tanzania imepiga hatua kubwa zaidi.

Alitaja eneo lingine walilokubaliana ni kuendeleza ushirikiano wa kimataifa na kikanda ili kuifanya jamii ya habari kuwa yenye manufaa endelevu, mifumo imara ya kisheria na kanuni zinazosaidia matumizi ya TEHAMA na kuifanya kuwa msingi imara katika kuwezesha sekta zingine.

Pia, walikubaliana masuala ya kitamaduni katika zama za kidijitali, jukumu la vyombo vya habari katika jamii ya habari na umuhimu wa uhuru wa kuzungumza ikiwamo athari za kimaadili kwa jamii kupitia TEHAMA.

Waziri Silaa alisema kikao hicho kinafanyika wakati tayari Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan, ameshazindua Mkakati wa Tanzania ya Kidigitali wa miaka kumi (2024-34), unaoonesha nchi itakavyojumuisha masuala ya TEHAMA kwenye uchumi na masuala ya kijamii.

Waziri Silaa alisema mkutano huo ni kwa ajili ya kufanya mapitio kuona maeneo 11 ambayo nchi za Afrika wamefikia na changamoto.

"Yapo mengi Tanzania imefanya mfano uwekezaji katika TEHAMA, ujenzi wa Mkongo wa Taifa, usimikaji minara ya mawasiliano, sheria mbalimbali zimetungwa kuhakikisha nchi inaendelea kushiriki na nchi nyingine duniani katika uchumi wa kidijitali," alisema.

Waziri Silaa alisema jarida la Muungano wa TEHAMA Duniani lililotoka mwezi Septemba, Tanzania imetajwa kama moja ya nchi 49 vinara katika ulinzi wa kimtandao na kwa nchi za Afrika na kuibuka namba moja.

Alisema si tu uwekezaji katika mifumo ya TEHAMA na miundombinu, vilevile katika utendaji nchi iko vizuri.

Waziri Silaa alisema mkutano huo umekuja wakati Tanzania imetangaza mkutano mkubwa utaokutanisha nchi taasisi zote za TEHAMA unaotarajia kufanyika kwa siku tano kuanzia Jumamosi wiki hii. Mkuu wa Idara ya Ubunifu na Teknolojia wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu Uchumi wa Afrika (ECA), Dk. Mactar Seck, alisema maeneo hayo 11 watayafanyia mapitio ya kina ili kuja na yatokanayo ambayo ni muhimu kwa mkutano ujao wa WSIS+20.

Alisema matokeo ya kikao kazi hicho yataandaliwa ripoti ya kina ya mapito iyakayotoa mapendekezo ya sera kwa ajili ya kuongeza utekelezaji wa WSIS barani humo.

## Mwinyi ataka wadau ukarabati Mji Mkongwe

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar inahitaji wadau zaidi kuunga mkono juhudi za kutunza, kuhifadhi na kuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar kutokana na umuhimu wake kwa uchumi wa nchi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, Dk. Mwinyi aliyasema hayo, Ikulu alipozungumza na ujumbe kutoka International National Trust Organization ya Uingereza iliyomweleza mafanikio iliyoyapata katika kulifanyia ukarabati jengo la "Customs House" lililoko Forodhani, maarufu kama jengo la Mizingani.

Alisema Mji Mkongwe mbali na kuwa eneo la urithi wa dunia, pia ni muhimu kwa kukuza uchumi wa Zanzibar kupitia sekta ya utalii kwa kuwa linatembelewa na wageni wengi.

Dk. Mwinyi alieleza kufarijika kwake kwa juhudi na hatua zilizochukuliwa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na Jumuiya ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe (JUHIMKO) kwa kulifanyia ukarabati mkubwa jengo la Mizingani.

Pia alisisitiza taasisi na wadau wengine kujitokeza kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuyahifadhi maeneo ya urithi kwa kuwa Mji Mkongwe una majengo mengi yanayohitaji ukarabati na kutunzwa kwa fedha na utaalamu.

Kuhusu mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo kuongezeka na kina cha bahari, Meneja Miradi wa International National Trust Organization, David Simpson, alisema ni changamoto inayoikabili miji mingi ya urithi duniani iliyoko pembezoni mwa bahari kama ilivyo kwa Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Kutokana na changamoto hiyo, aliahidi taasisi yake kuendeleza ushirikiano na Zanzibar kuhakikisha Mji Mkongwe unabaki kwenye ramani ya dunia. Alisema taasisi hiyo imefanya kazi katika nchi 102 duniani kwa kukarabati miji mikongwe.

Zaidi ya paundi 80,000 (takriban Sh. milioni 240) zilitumika kulifanyia ukarabati mkubwa jengo la Mizingani chini ya ufadhili wa Mfuko wa Baraza la Urithi la Uingereza.

Ujumbe huo uliosheheni wataalamu wa uhifadhi wa miji ya urithi, ukingozwa na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, ulijumuisha taasisi za uhifadhi miji ya urithi kutoka Uingereza, Jordan, Misri na Uganda.

# Majaji waagizwa kushiriki maboresho sheria WCF

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAJAJI wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania wameagizwa kushiriki kutoa ushauri wa kisheria kwa ajili ya maboresho ya Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Agizo hilo limetolewa na Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Juma, wakati akifungua kikao kazi cha majaji wa mahakama hiyo na WCF jijini hapa jana.

Prof. Juma, alisema ushauri wa majaji hao, utasaidia pamoja na mambo mengine, kuongeza tija na ufanisi kwenye mnyororo wa utoaji haki kwa wafanyakazi wanaopata madhila wakiwa kazini.

Kutokana na umuhimu huyo, aliwataka majaji hao kusaidia upatikanaji wa sheria endelevu ya mfuko huo.

**kwenye mnyororo wa utoaji haki kwa wafanyakazi wanaopata madhila wakiwa kazini.**

"Tufahamu ushirikiano kati ya Mahakama, Mfuko wa Fidia na wadau wote katika mnyororo wa haki za wafanyakazi nchini ni sehemu ya malengo ya kikatiba ya ustawi wa jamii unaolenga kuhakikisha haki za wafanyakazi zinazingatiwa na kulindwa ipasavyo," alisema Jaji Mkuu.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, aliwahakikishia majaji hao kuwa mapendekezo wanayotoa ya uboreshaji wa sheria hizo yatapokelewa na kufanyiwa kazi.

Mapema, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema ushirikiano baina ya mfuko huo na Mahakama ya Tanzania, umechangia katika maboresho kadhaa kuhusu Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi na michango ya majaji.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati, Khalifan Matipula (kushoto), akimpongeza Mwenyekiti mpya wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Elisha Mnyawi, baada ya kuchaguliwa, mjini Babati juzi. Katikati ni mdau wa maendeleo, Hans Nkya. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mchengerwa alitolea uvivu Jiji

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeagiza Halmashauri ya Jiji la Arusha kutumia fedha za mapato ya ndani Sh. bilioni 2.1 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Esso-Longdon ili kuondoa adha kwa wananchi kukosa usafiri kutokana na ubovu.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wake, Mohamed Mchengerwa baada ya kukagua barabara hiyo inayopita Kata ya Sokoni I na Unga Ltd kufuatia malalamiko ya wakazi wa jijini hapa kuwa ni mbovu na kero kwa kukosa usafiri. Mchengerwa baada ya kukagua barabara hiyo barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 1.8 , alisema hakuna haja kwa jiji jilo kuhifadhi fedha kwenye akaunti zake, wakati wananchi wanahitaji huduma bora, ikiwamo kuwa na miundombinu ya usafiri yenye uhakika.

"Kutokana na hiki nilichokiona, naelekeza sasa tumieni fedha za mapato ya ndani kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami, pia ongeeni na wananchi walioko pembezoni," alisema na kuongeza kuwa: "Msiwaogope waambieni, wataathiriwa na mradi wa ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo waangalie namna bora ya wao kupisha ili kutoa fursa kwa barabara kujengwa kwa kiwango cha lami na kuongezewa thamani."

# NBS yaja kivingine kwa utafiti

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imesema kuanzia sasa utafiti utakuwa ukifanyika kila mwaka kwa ajili ya kusaidia serikali kupima matokeo ya mikakati ya kitaifa kwa umma na kurekebisha maeneo yenye kasoro.

Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Magreth Magana, aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akizungumza na maofisa habari wa halmashauri na mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

Magana, kabla ya mabadiliko hayo, utafiti huo ulikuwa ukifanyika kila baada ya miaka mitano na kusisitiza kuwa kuanzia sasa utafanyika kila baada ya mwaka mmoja pia kuwasaidia wadau kutekeleza malengo yao.

Alisema msisitizo umewekwa kuimarisha uwezo wa taasisi zinazozalisha takwimu za kiutawala ili ziwekwa kiwango bora na kutumika kufanya maamuzi.

Awali, Meneja wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Uratibu wa Takwimu wa NBS, Mwanaidi Mahiza, alisema baada ya kujengewa uwezo maofisa habari hao, wanataka kuona mabadiliko chanya katika kuripoti mambo ya kijamii na ya kitaifa.

Kwa mujibu wa Mwanaidi, NBS inatarajia mabadiliko makubwa katika kusambaza taarifa za kijamii na kiuchumi kwa wananchi.

Alisema NBS imeamua kuwajengea uwezo wa namna ya kutafsiri takwimu kwa wananchi ili waweze kuelewa kwa urahisi.

Akifungua kikao kazi hicho, Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Maryam Muhaji, alisema habari ni msingi wa haki za binadamu, hivyo kuripoti ambayo siyo sahihi ni ukiukaji wa haki za binadamu.

"Kila mtu anapoamka asubuhi anatumia takwimu na hata tunapobeba viumbe tumboni mpaka tunajifungua tunakuwa tumetumia takwimu," alisema.

# Maofisa halmashauri wapigwa msasa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI imeanza kuwanoa maofisa wake wa halmashauri Tanzania Bara kwa ajili ya kuimarisha huduma na kuboresha matumizi ya rasilimali fedha.

Akifungua mafunzo hayo yanayoendeshwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) jana, Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Mussa Misaile, alisema serikali imedhamiria kupeleka huduma bora kwa wananchi.

Akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Ofisa Mipango na Uratibu wa Jiji la Arusha, Apolinary Seiya, Masile, alisema washiriki hao watajengewa uwezo kufanya ufuatiliaji wa kina na tathmini ya miradi, sera na mipango ya serikali katika halmashauri hizo za jiji, manispaa na wilaya kwa Bara.

"Serikali imetumia wataalamu bobezi kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania wanatoa mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini kwa maofisa kutoka katika idara za serikali kuu, taasisi na mashirika ya umma na serikali za mitaa.

"Haya ni mafunzo ya awamu ya kwanza, kwa maofisa kutoka serikali za mitaa; ikizingatiwa ziko karibu na wananchi, hivyo uboreshaji wa huduma kupitia mafunzo haya ni jambo la muhimu," alisema Seiya na kuongeza kuwa:


"Serikali katika ngazi hiyo, imeanzisha vitengo vipya vya ufuatiliaji na tathmini, hivyo mafunzo hayo yanakwenda kuimarisha utawala bora kwenye maeneo husika na kusaidia kupanga vipaumbele vya miradi ya maendeleo serikalini."

Mkurugenzi wa Kitengo Maalum cha Ushauri wa Kitaamu OUT, Dk. Emmanuel Mallya, alisema mafunzo hayo pia yanalenga kuboresha uwezo wa maofisa hao wa serikali za mitaa kuimarisha huduma na kuboresha matumizi bora ya rasilimali fedha.

Ofisa Mipango wa Jiji la Dar es Salaam, Happiness Nchimbi, aliishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na chuo hicho, kufanikisha mafunzo kwa maofisa mipango, wachumi, na watakwimu.

Mafunzo hayo yanalenga kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwa taasisi za serikali, mashirika ya umma, serikali kuu na serikali za mitaa za Tanzania Bara.

Awamu ya pili inatarajiwa kufanyika Oktoba 21 hadi Oktoba 25, mwaka huu jijini Dodoma.



**Na Thobias Mwanakatwe,**

IKUNGI

MKUU wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Thomas Apson amekemea lugha chafu zinazotolewa na baadhi ya wauguzi hospitalini, vituo vya afya na zahanati za serikali wilayani hapa na kusababisha wagonjwa kufa kwa kukosa huduma.

Maofisa wa idara mbalimbali za Halmashauri ya wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, wakizungumza na mkazi wa kijiji cha Majereko, Melea Obed ambaye ni mlemavu wa viungo aliyenufaika na msaada kutoka shirika lisilo la kiserikali la Brac Maendeleo Tanzania, uliomwezesha kuwa mjasiriamali na kuachana na kazi ya kuombaomba mitaani, walipomtembelea nyumbani kwake juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

**Alisema hatua hiyo itasaidia mtu kusafiri kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kwa kutumia gesi asilia kwa sababu ni rafiki kwa mazingira**

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania, Dk. Francis Alfred (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Thomas Bwana (kushoto), wakishiriki uzinduzi wa



## HABARI DODOMA

# EWURA yafungua milango malalamiko maji, umeme, mafuta

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetoa wito kwa wananchi kuwasilisha malalamiko kwa kukosa huduma bora ili yapatiwe ufumbuzi.

Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa EWURA, Tobietha Makafu, alitoa wito huo jana jijini hapa wakati akielezea Mamlaka hiyo ilivyojipanga kuwahudumia wadau wake katika Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyoanza Oktoba 7, mwaka huu.

Makafu alisema kuwa; "Mathalani mtu amejenga nyumba yake, amelipia huduma ya kuunganishiwa umeme au maji, lakini unapita muda mrefu bila kupata huduma hiyo, tunakusihi leta malalamiko hayo kwetu na sisi EWURA tutahakikisha unapata huduma hiyo kwa mujibu wa utaratibu uliopo kisheria," alisema.

Vilevile, alisema mteja anapopelekewa ankara ya maji kama hajaridhiki nayo, au msoma mita anakadiria bila kusoma mita, mteja anapaswa kuwasilisha suala hilo kwa mamlaka ya maji na kwamba kama hakupata atoe taarifa EWURA.

"Sisi tutahakikisha tunamsaidia kupata mustakabali wa suala hilo," alisisitiza Makafu.

> **"Bidhaa ya mafuta inatoka haraka hivyo ni muhimu kuwasiliana nasi kwa haraka kabla mafuta yanayohusika haijaisha ili wataalamu wa EWURA waweze kufanya uchunguzi...**

Kuhusu malalamiko kuhusu mafuta, alisema inapotokea mteja ameweka yakasababisha chombo kuharibika, anapaswa kuwasilisha kwa msimamizi wa kituo cha mafuta na endapo hatapata ufumbuzi EWURA ndani ya siku saba ili yashughulikiwe.

"Bidhaa ya mafuta inatoka haraka hivyo ni muhimu kuwasiliana nasi kwa haraka kabla mafuta yanayohusika haijaisha ili wataalamu wa EWURA waweze kufanya uchunguzi na kumwezesha mteja kupata haki yake," alisema Makafu.

Kuhusu wiki hiyo, alisema katika Ofisi ya Makuu Makuu ya EWURA, wateja wamepata fursa ya kuhudumiwa moja kwa moja na Mkurugenzi Mkuu, Dk. James Andilile na Wakurugenzi wa Idara na kwa Ofisi za Kanda, watendaji wametoka ofisini kuwafuta wadau wao.

"Mathalani Kanda ya Magharibi, wanatoa huduma katika viwanja vya shule ya msingi Uyui mkoani Tabora, hivyo tumejipanga kuhakikisha kila mwenye changamoto anapata huduma," alisema.

Alisema wamejipanga kuhakikisha kila mwananchi anaendelea kupata huduma bora za umeme, mafuta, gesi asilia, maji na usafi wa mazingira.




Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bestina Magutu, wakati wa maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima katika viwanja vya Chipukizi, mjini Tabora jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# AAFP yashauri vyama kuteua wagombea wanaokubalika

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

CHAMA cha Wakulima (AAFP) kimevishauri vyama vya siasa nchini kuteua wagombea wanaokubalika kwa wananchi ili wawachague katika chaguzi zijazo na wawaletee maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Chama hicho Taifa, Mark Mhemella, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzingatiaji demokrasia unaofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kuelekea kwenye uchaguzi huo wa wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji.

Alisema chama hicho kimetoa ushauri huo ili kuondokana na mtindo wa baadhi ya vyama kupenyeza majina ya watu wanaowataka ili wagombea na kushinda kwa maslahi binafsi, hivyo kushindwa kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema chama hicho kinatarajia kuona uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na mkuu mwakani utakuwa wa haki na huru kwa vyama vitakavyowateua wagombea wanaokubalika kwa wananchi ili kuendana na falsafa ya Rais ya R4.

"Tunampongeza Rais kwa kusimamia demokrasia nchini, hii itawapa nafasi kubwa wananchi kuwachague viongozi wanaowataka wenyewe kupitia falsafa ya R4, pia tunawaka viongozi wetu kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, kata, vijiji hata mitaa kushiriki ipasavyo kwenye uchaguzi huu ili kupata idadi kubwa ya uwakilishi katika maeneo mbalimbali," alisema huku akitumia fursa hiyo kutangaza mpango wa chama hicho kushiriki katika uchaguzi huo mitaa na vijiji unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Chama hicho Wilaya ya Dodoma, Exsavery Mapunda, aliwaomba viongozi wa siasa kuacha tabia ya kuchagua watu wanaowataka kuwaweka madarakani badala ya wale wanaopendekezwa na wananchi.

Mapunda, alisema baadhi ya viongozi waliopewa dhamana ya kupitisha majina ya wagombea wamekuwa na utashi wa kuwachagua wanaowataka ili kulinda maslahi yao.

"Tabia hiyo ya viongozi ya kujipangia safu zao za uongozi tofauti na wanaowataka wananchi kuna hatari ya Taifa kukosa wabunge, madiwani na wenye viti wa mitaa na vijiji wazalendo," alisema.

Mwenyekiti huyo, alisisitiza kuwa tabia hiyo itawakatisha tamaa wananchi kuvipenda vyama vyao na kutoshiriki katika chaguzi nchini, hivyo kukosa viongozi watakaowaletea maendeleo.

# Wanachama wakumbushwa kuhakiki michango NSSF

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WANACHAMA wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wametakiwa kujenga utamaduni wa kufuatilia na kuhakiki taarifa za michango yao mara kwa mara wakiwa kazini badala ya kusubiri kustaafu.

Meneja wa NSSF Mkoa wa Singida, Oscar Kalimilwa, alitoa rai hiyo juzi wakati ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja mwaka huu mkoani hapa.

"Tunatambua mchango mkubwa wa wateja wetu katika kuwezesha mfuko wetu kuendelea kufanya shughuli zake kuu nne," alisema na kuzitaja kuwa ni uandikishaji wanachama, ukusanyaji michango, ulipaji mafao na uwekezaji na kuwaomba wanachama wao kuhakiki michango yao mara kwa mara.

Kalimilwa, alisema mfuko huo hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha uliopita wa 2023/24 ulikuwa na wanachama 1,354,985 na waajiri 43,430 na kuandikisha wanachama wapya 291,266.

Alisema kwa mwaka 2024/2025 wamelenga kuandikisha wanachama wapya 324,321 na kwamba mfuko umekamilisha taratibu zote za uanzishwaji wa mfumo wa ufunguzi na malipo ya mafao kupitia mtandao kwa kuanza baadhi ya mikoa.

"Huduma hii inatoa fursa kwa wanachama waliopo mbali na matawi yetu kuweza kufungua matawi mahali popote walipo, kufuatilia maendeleo ya ulipaji na hatimaye kulipwa kwa mujibu wa kanuni za ulipaji wa mafao," alisema.

Aliongeza kuwa wajibu wa watumishi mfuko huko ni kuhakikisha wanafikia matarajio ya wateja na wadau wao ikiwa ni pamoja na wastaafu wanaopokea mafao, wanachama waliopo sasa na baadaye.

Kalimilwa alisema mfuko umeboresha mfumo wa sekta isiyo rasmi mahususi kwa wanachama wote walioajiriwa na umeandaa skimu kwa wafanyakazi katika sekta rasmi ili kujichangia kwa hiari kupitia skimu hiyo.

Alisema skimu hizo, NISS na SS zinalenga kupanua wigo wa huduma za hifadhi ya jamii nchini na kuchangia kuondoa umaskini kwa wananchi.

Ofisa NSSF Mkoa wa Singida, Kenneth Kalinjuma, alisema mfuko huo umepanua wigo wa hifadhi ya jamii kwa kuyafikia makundi yote ya wananchi waliojiajiri wakiwamo waendesha bodaboda, bajaj, mama na baba lishe, wakulima na wafugaji ambao wanafika kujiandikisha kwa ajili ya kuweka akiba zao ambazo zitawasaidia baadaye.

Wiki hiyo ilianzishwa kimataifa mwaka 1987 kwa lengo la kutambua umuhimu wa huduma bora kwa wateja na juhudi za wafanyakazi wanaotoa huduma bora kwa wateja.



# WAVIU: TARURA imeboresha maisha yetu

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WATU wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) wilayani hapa Mkoa Njombe, wameushukuru Wakala wa Barabara wa Mijini na Vijijini (TARURA) kwa kuwapa zabuni za ujenzi wa miradi na kuboresha maisha yao kutokana na kipato.

Hayo waliyasema juzi mbele ya viongozi wa Wizara ya Miundombinu kutoka nchini Sierra Leone baada ya kumbelea vikundi viwili, kikiwamo Tujipime kwa lengo la kujifunza jamii inavyoweza kushirikishwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Walisema zabuni hizo zimewawezesha wanachama wa kikundi hicho kuinua hali ya maisha yao, uchumi, maendeleo kwa kujenga nyumba na kununua mashamba na viwanja.

Mmoja wa wanachama wa Tujipime, Aulelia Theodori, alisema miradi hiyo pia imewasaidia kupata fedha za kusomesha watoto wao kuanzia elimu ya msingi hadi chuo kikuu.

"Kwa kweli tunafarijika tupo pamoja tunafanya kazi, tumejenga nyumba tumenunua mashamba, viwanja mpaka sasa hatujapata changamoto yoyote na tumefanikiwa kuwa na vikundi vya kukopeshana na kusaidiana katika shida na raha," alisema Theodori.

Mwenyekiti wa Kikundi hicho, Melsela Mlelwa, alisema wanaishukuru TARURA kwa kuwasaidia kupata kazi kwa wakati na bila ya usumbufu wowote.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga alisema anajivunia kuwa na jamii iliyoweza kutengeneza umoja na kutambua fursa zilizoko.

"Kama hapa tumeona madaraja yalivyojengwa kwa ubora kwa kushirikiana na TARURA, hivi ni vikundi tu ambavyo vimeweza kupewa mafunzo ikiwa ni njia nzuri ya serikali kurudisha kwa jamii na jamii imedhihirisha kuwa inaweza kunusa na kuzitambua fursa zilizoko," alisema Kamonga.

**"Wilaya yetu imeweza kupokea ugeni kutoka wizara ya miundombinu waliokuja kujifunza namna ya ushirikishwa wa jamii katika miradi ya maendeleo huwezi ukaigilizia kwa mtu anayepata**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Olivanus Thomas, alisifu ujio wa wageni hao kwa ajili ya kujifunza ushirikishwaji wa jamii katika miradi ya maendeleo.

"Wilaya yetu imeweza kupokea ugeni kutoka wizara ya miundombinu waliokuja kujifunza namna ya ushirikishwa wa jamii katika miradi ya maendeleo huwezi ukaigilizia kwa mtu anayepata sifuri ndio maana ujio wa wageni wetu una maana yakuwa kuna kitu wamekiona katika ardhi ya Tanzania hususani Ludewa ndio maana leo hii tuko nao hapa wakijifunza," alisema Thomas.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Matengenezo ya Barabara kutoka Sierra Leone, Mohamed Kallon, alisema amefurahishwa na wakala huyo kuwa na mpango shirikishi wa vikundi vya jamii kwenye miradi ya barabara.

"Nimevutiwa na jitihada za kikundi cha wanaoishi na virusi vya Ukimwi ambao licha ya kufanya kazi za kuboresha barabara vijijini, nimependa kusikia mnashughuli nyingine kama ufugaji, kilimo na kukopeshana fedha," alisema Kallon.

Meneja wa TARURA Ludewa, Mhandisi Butene Jilala, alisema kuna vikundi 52 vya nguvu kazi vinavyotumia teknolojia na kimojawapo kinaitwa 'Tujipime' ni kikundi ambacho tumeanza kufanya nacho kazi mwaka 2020.

Tujipime chenye wanachama 22 wanaoishi na VVU kilisajiliwa mwaka 2019 na kuanza rasmi kazi 2020 za miradi ya TARURA Ludewa.



Mafundi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Mara, wakishusha baadhi ya mabomba ili kuyatandaza katika vijiji vya Wilaya ya Musoma Vijijini, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wahamasishwa kujiandikisha daftari mpigakura

**Na Eizabeth John,** LUDEWA

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwenye daftari la mpigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa ili wapate sifa ya kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo kwenye maeneo yao.

Mtaka aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Mundindi wilayani hapa.

Mtaka alisisitiza kuwa ili kila mwananchi aweze kupata fursa ya kupiga kura ni lazima ajiandikishe kwenye daftari hilo.

"Wananchi hakikisheni mnajiandikisha kwenye daftari la wapigakura kuanzia oktoba 11 hadi 20, mwaka huu, vyama vya siasa tuleteeni wagombea wazuri kwa sababu serikali tutasimamia uchaguzi wa huru na haki," alisema.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa mkoa huo, Julius Peter, alisema ili mwananchi apate fursa ya kupiga kura ni lazima ajiandikishe kwenye daftari hilo. "Rai yangu wananchi wa Mundindi kwa umoja wetu tujitokeze kwa wingi, twende tukajiandikishe kwenye daftari hilo na uchaguzi kwa maana uchaguzi ni namba, uchaguzi ni takwimu," alisema Peter.

Aliwataka wananchi na wanachama wa chama hicho kutembea kifua mbele na kueleza mafanikio ambayo yamefanyika katika maeneo yao.

"Jambo jingine la kumpa zawadi Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa sababu mambo ambayo ametutendea ni makubwa sana kwenye kata yetu, Lazima sisi wanaCCM tuyasemee mafanikio haya yaliyotekelezwa na serikali ya awamu ya sita," alisema. Baadhi ya wakazi wa kata hiyo, akiwamo Clementina Mkinga, alisema kujiandikisha ni jambo muhimu kwa sababu ndiyo fursa pekee itayompa mwananchi fursa ya kupiga kura.

Mkazi huyo alitoa rai hasa kwa vijana kujitokeza na kugombea uenyekiti wa mtaa, kijiji na kitongoji katika uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika nchini mwezi ujao.

## Wakulima wahaha kusaka soko la mazao

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa Kata ya Kitandililo Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani hapa Mkoa wa Njombe, wameiomba serikali kutafuta soko la uhakika la mazao hususan mahindi ili wauze kwa tija na kuongeza kipato.

Ombi hilo walilitoa juzi wakati wakizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa msimu mpya wa kilimo wa mwaka 2024/2025 uliofanyika mjini hapa.

Walisema kwa sasa mazao hayo hususani ya mahindi hailingani na gharama za uzalishaji kwa kuuza debe lenye ujazo wa kilo 20 kwa shilingi 6, 000.

Mmoja wa wakulima hao, Erasto Ndulundu, aliiomba serikali kuhakikisha wadau wa pembejeo za kilimo hasa mbegu na mbolea wanafikisha vijijini na kuwaondolea gharama kubwa kufuata mjini.

Veronica Tweve, alisema wanatumia gharama kubwa katika kilimo na kwamba kwa kukosa soko la uhakika, wanalazimika kuuza mazao yao kwa hasara.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Peter Muro, alisema ili kuhakikisha wakulima wanapata tija, wataalamu wameanza kupima afya ya udongo bure na kuwataka wakulima kuhuisha taarifa zao kwa lengo la kupata mbolea za ruzuku.

Diwani wa Kata ya Kitandililo, Imani Fute, aliwataka wakulima kuachana na kilimo cha mazoea na kupata elimu kwa wataalamu wa kilimo.

Fute, aliwataka mawakala kuacha tabia ya kuwazuia wakulima pembejeo zisizo na ubora ili wapate mazao ya kutosha.

Baadhi ya wadau wa kilimo, akiwamo Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya One Acre Fund ya Njombe, Braiton Willa, alisema watahakikisha wanafikisha pembejeo hizo kwa wakati vijijini ili wakulima wapate kwa gharama nafuu.





# Matukio ya ukatili yazidi kuongezeka



## HABARI KANDA YA ZIWA



Mbunge wa Jimbo la Solwa, Ahmed Salum (wa pili kulia), akibebeshwa nyoka aina ya chatu na kikundi cha ngoma Kata ya Tinde, wilayani Shinyanga, walipotumbuiza katika mkutano wa Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 'Maji Ziwa Victoria si salama'

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka huu, Godfrey Nzava, amesema maji ya Ziwa Victoria si salama kwa matumizi ya binadamu na kuitaka serikali kuongeza juhudi kutibu maji kabla ya kufikisha kwa wananchi.

Mzava alitoa kauli hiyo juzi baada ya Mwenge huo kukagua utekelezaji wa mradi wa kuondoa na kutibu maji taka uliopo Gereza Kuu la Butimba na wa chanzo cha maji Butimba, wilayani Nyamagana Mkoa wa Mwanza.

"Maji ni huduma ambayo haina mbadala, serikali kwa kutambua hilo ikaamua kufanya uwekezaji wa kutafuta majawabu ya tatizo la maji safi na salama kwa wananchi wa Jiji la Mwanza na viunga vyake, na wameanza kupata maji tumetembelea, tumeona kazi imetekelezwa vizuri, " alisema Mzava.

**"Maji ni huduma ambayo haina mbadala, serikali kwa kutambua hilo ikaamua kufanya uwekezaji wa kutafuta majawabu ya tatizo la maji safi na salama kwa wananchi wa Jiji la Mwanza....**

Alisema kazi ya kutibu maji taka yanayozalishwa viwandani, nyumbani na maeneo mengine ya biashara lazima ifanyike kwa makini ili yasiendelee kuzagaa juu ya uso wa dunia, kuharibu mazingira na kusababisha matatizo ya afya kwa jamii.

Meneja Miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Celestine Mahubi, alisema mradi huo wa kuondoa na kutibu maji taka wanautekeleza kwa gharama ya Sh. bilioni 1.96 ili kulinda chanzo cha maji cha ziwa hilo.

Kuhusu mradi wa chanzo cha maji Butimba, alisema umegharimu Sh. bilioni 71.69 na kukamilika kwa asilimia 100.

Alisema chanzo hicho kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 48 za maji kwa siku na baadhi ya wananchi wameanza kunufaika.

# Mwassa aibua kiini lishe duni Kagera

**Na Restuta Damian,** KAGERA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwassa, amesema wakazi wa mkoani hapa hawana utamaduni wa matumizi sahihi ya vyakula wanavyozalisha na kusababisha kuwa miongoni mwa mikoa yenye tatizo la lishe duni nchini.

Mwassa alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yanayofanyika kitaifa mkoani hapa kuanzia Oktoba 10 hadi 16, mwaka huu.

Alisema Kagera unazalishwa ndizi, maharage, mahindi, karanga, mihogo, viazi vitamu na lishe kwa wingi, lakini tatizo ni matumizi kwa wakazi wake.

"Kinachofanya lishe kutokuwa vizuri ni pamoja na wananchi kutotumia vyakula hivyo kwa usahihi, kula milo isiyo kamili na kuuza mazao ili kujipatia kipato," alisema.

Kuhusu maadhimisho hayo, Mwassa alisema, mkoa umejipanga kushirikiana na Wizara ya Kilimo kufikisha maudhui kwa wananchi nchini na kuhimiza ulaji na kulima vyakula vinavyohitajika katika mwili wa binadamu.

Katibu Tawala Msaidizi Upande wa Uchumi na Uzalishaji wa mkoa huo, Isaya Tendega, alisema hali ya uzalishaji wa vyakula mkoani hapa bado ipo chini ikilinganishwa na mahitaji, hivyo kulazimu chakula kingine kutoka nje ya mkoa.

Pendega, alisema uzalishaji wa vyakula ndani ya mkoa ni tani milioni 3.4 na matumizi milioni 7.7 huku zaidi ya 2.7 zikiuzwa nje.

# Mbunge ajinasua kijiji kukosa huduma za afya

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKAZI wa Kijiji cha Mwasele wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga wamemtaka Mbunge wao wa Kishapu, Boniphace Butondo awaeleze sababu ya serikali kushindwa kujenga kituo cha afya katika maeneo.

Wakazi hao, akiwamo Said Hamis, wakizungumza juzi kwenye mkutano wa mbunge huyo uliofanyika Mji wa Mhunze, walidai kukosekana kwa kituo hicho kunasababisha maisha yao kuwa hatarini kwa watakaohitaji matibabu ya dharura baada ya kuugua ghafla.

Hamisi, alisema serikali imekuwa ikijenga vituo vya afya, zahanati na hospitali kwenye maeneo mengine na kukiruka kijiji chao, kitendo kilichowalazimu kumhoji mbunge wao ili kupata majibu. Akizungumza katika mkutano huo, Mbunge Butondo, aliuagiza uongozi wa kijiji hicho kushirikiana na diwani wa kata yao kutafuta eneo la kujenga zahanati. Aliahidi kutoa mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya hatua za awali za ujenzi na zahanati hiyo na kuwataka wakazi hao kumbana mkurugenzi wa halmashauri yao kukamilisha ukifika hatua ya renta.

# Wauziwa ndoo 1,000/- kwenye tingatinga

**Na Judith Julius,** NGARA

WAKAZI wa Kata ya Nyamiaga wilayani hapa Mkoa wa Kagera wamedai hawana huduma ya majisafi na salama katika maeneo yao tangu mwaka 1974.

Wakazi hao walitoa kilio hicho juzi katika mkutano wa Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoro, uliofanyika Kijiji cha Kumuyange.

Mmoja wa wakazi hao, Magreth Gwassa, alidai wamekuwa wakitumia maji yasiyosalama kwa afya zao ya kwenye tingatinga kwa kuuziwa ndoo kwa Sh.1,000 na kusababisha baadhi yao kukumbwa na magonjwa ya tumbo.

George Ngeze (66), alidai tangu kuzaliwa kwake ameshuhudia familia nyingi zikitumia maji yaliyopo kwenye tingatinga ambayo si salama kwa afya zao.

Diwani wa Kata hiyo, Eustasi Majita, alithibitisha kata hiyo kukosa maji safi na wakazi wake kutumia muda mwingi kusaka na kushindwa kushiriki katika shughuli zao za kiuchumi.

Akijibu kero hiyo, Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani hapa, Simon Ndyamkama, alisema wanajenga vyanzo viwili vya maji kwa ajili ya kusambaza maji safi na salama katika kata hiyo.

Ndyamkama, alivitaja vyanzo hivyo kuwa ni matangi mawili yenye ujazo wa lita 25,000 na 75,000 kwa gharama ya zaidi ya Sh.bilioni 1.6 ili kuwahudumia wakazi hao wakati wote.

Alisema mamlaka hiyo pia inatarajia kujenga mtandao wa maji na kutengeneza kituo cha kuchota maji kwa kadi ya malipo ya kabla kwa ajili ya wakazi hao.

Mbunge Ruhoro alimwagiza Meneja wa RUWASA kumsimamia mkandarasi ili akamilishe kwa wakati mradi huo na kutekeleza adhima ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani. "Mradi huu ukamilike ndani ya miezi sita kama ilivyopangwa kwani wananchi wameteseka kwa muda mrefu, wanahitaji kupata huduma hiyo muhimu," alisema.



# Waziri awabana maofisa ustawi jamii kesi udhalilishaji kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

MAOFISA ustawi wa jamii wa mikoa na wilaya katika Kisiwa cha Pemba, wametakiwa kufuatilia kesi za udhalilishaji wa kijinsia na kuhakikisha zinafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Wito huo ulitolewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, wakati akizungumza na viongozi na maofisa hao kisiwani hapa.

Juma, alisema serikali imejipanga kuhakikisha kesi zinazofikishwa mbele ya vyombo vya sheria zinafanyiwa kazi na kushughulikiwa kwa haraka ili kutokomeza vitendo hivyo kisiwani hapa.

Alisema kumekuwa na malalamiko ya wananchi ikiwamo wazazi kutokana na tatizo la kuchelewa na kushughulikiwa kesi dhidi ya vitendo hivyo kwenye vyombo hivyo kuanzia Jeshi la Polisi hadi mahakama.

**Alisema kumekuwa na malalamiko ya wananchi ikiwamo wazazi kutokana na tatizo la kuchelewa na kushughulikiwa kesi dhidi ya vitendo hivyo kwenye...**

Hata hivyo, Waziri huyo alionyesha kufurahishwa na kasi ya mahakama kushughulikia kesi hizo na kutoa hukumu haraka.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Anna Athanas Paul, alisema wanafanya tathmini ya mwenendo wa kesi hizo ili kubaini ongezeko la matukio hayo.

Anna, alisema matukio ya kesi hizo, yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku licha ya kutolewa elimu jinsi ya kupambana nayo inayotolewa kupitia vyombo vya habari.

Ofisa Mwandamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Ahmed Rashid Ali, alisema wanatekeleza mradi wa jinsia ili kufahamu athari za matukio hayo na kukabiliana nayo.

Alisema elimu dhidi ya matukio hayo, shirika hilo litahakikisha inatolewa zaidi kuanzia ngazi ya shina hadi vijijini.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abulla, akikata utepe kuzindua Mfumo wa Taarifa za Elimu Shuleni (SIS), mjini Zanzibar juzi. Wengine ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa na Mkurugenzi Mkaazi wa USAID Tanzania, Craig Hart. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mfumo kuboresha utendaji sekta ya elimu Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imezindua mfumo wa taarifa za elimu kwa kutumia kompyuta lengo la kuboresha utendaji wa sekta ya elimu visiwani hapa.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alisema kuwa mfumo huo utaleta mabadiliko na kutatua changamoto ikiwamo kuchelewa utoaji maamuzi ya sera na utawala kwa wakati.

"Mfumo huu mpya utawezesha kazi za ukusanyaji, uchambuzi na matumizi ya takwimu kufanyika kwa urahisi, ufanisi mkubwa na kupunguza gharama," alisema Hemed.

Alisema serikali inakusudia ifikapo Januari mwakani shule ziendeshwe kwa mkondo mmoja.

Alisema kwa sasa asilimia 67 ya shule za msingi zinaendeshwa kwa mkondo mmoja na sekondari asilimia 86.

Alisema mfumo huo ni nguzo muhimu kuyafikia malengo ya mageuzi ya elimu nchini na kwamba serikali imewekeza fedha nyingi hasa katika sekta ya elimu. Hemed, alisema serikali pia imeweka malengo ya kufuta daraja sifuri katika ufaulu wa mitihani ya taifa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema serikali iwekeza mikakati ya kuboresha mifumo maalum ya kutoa taarifa ili kupata uelewa wa kuwafundisha na kufikia malengo ya ufaulu kwa wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari.

Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), Dk. Massoud Mohd Salim, alisema mfumo wa taarifa za elimu utasaidia kuimarisha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi.

Dk. Salim, alisema ili mfumo huo uweze kufanya kazi, kunahitajika ushirikiano kati ya wizara hiyo, walimu, wazazi na wadau wa elimu nchini kufikia mageuzi ya elimu Zanzibar.

Akiwasilisha taarifa ya mfumo huo, Naibu Katibu Mkuu Utwala wa Wizara ya Elimu, Khalid Wazir, alisema mfumo huo utasaidia ukaguzi, uandaaji wa mitihani na uchakataji wa taarifa za walimu na wanafunzi watoro ili kila mtoto apate haki yake ya msingi ya kusoma.

# Dk. Mwinyi, Gavana Comoro wateta

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema wakati umefika kurejesha diplomasia ya uchumi na kuendeleza biashara baina ya Zanzibar na ya Comoro ili kudumisha ushirikiano baina ya nchi hizo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar wakati akizungumza na Gavana wa Jiji la Moroni, Visiwa vya Ngazija, Ibrahim Mzee na ujumbe wake baada ya kuwasilisha nia ya kukuza ushirikiano baina nchi hizo.

Dk. Mwinyi, aliushauri ujumbe huo kurejesha makundi ya wafanyabiashara wa nchi hiyo kuja Zanzibar kuangalia fursa za biashara na uwekezaji kama ilivyokuwa miaka iliyopita.

Alisema ni vyema pande mbili hizo kufikiria namna ya kurejesha huduma ya usafiri wa vyombo vya baharini ili kuwanufaisha wananchi na fursa za biashara na jamii.

Mwinyi aliutaka ujumbe huo kuweka utaratibu maalumu kwa walimu wa Zanzibar kwenda Comoro kufundisha Kiswahili au wa nchi hiyo kuja visiwani Zanzibar kujifunza lugha hiyo kwa sababu zinashabihiana.

Gavana Mzee alisifu kasi ya mabadiliko na maendeleo ya Zanzibar na kusema nchi yake ina kitu cha kujifunza kama vilivyofanikiwa nchi hiyo.

Alitumia fursa hiyo, kumualika Mwinyi kuzuru visiwa vya Ngazija kwa lengo la kubadilishana uzoefu kwenye nyanja za maendeleo.

Eneo jingine aliloligusia ni kuimarisha ushirikiano wa karibu baina ya Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wakulima na Wenye Viwanda Zanzibar na Comoro ili kukuza biashara baina yao.

Akiambatana na ujumbe huo, Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Muhammed Mussa, alisema utakuwapo Zanzibar kwa siku tatu na kuwa na mazungumzo ya ushirikiano baina yao na Manispaa ya Jiji la Moroni.

Ujumbe huo utakuwa na siku maalum ya kutembelea Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao ni mji wa urithi unaotambulika na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa kwa lengo la kukuza ushirikiano.



## HABARI KANDA YA ZIWA



Mbunge wa Jimbo la Solwa, Ahmed Salum (wa pili kulia), akibebeshwa nyoka aina ya chatu na kikundi cha ngoma Kata ya Tinde, wilayani Shinyanga, walipotumbuiza katika mkutano wa Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 'Maji Ziwa Victoria si salama'

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka huu, Godfrey Nzava, amesema maji ya Ziwa Victoria si salama kwa matumizi ya binadamu na kuitaka serikali kuongeza juhudi kutibu maji kabla ya kufikisha kwa wananchi.

Mzava alitoa kauli hiyo juzi baada ya Mwenge huo kukagua utekelezaji wa mradi wa kuondoa na kutibu maji taka uliopo Gereza Kuu la Butimba na wa chanzo cha maji Butimba, wilayani Nyamagana Mkoa wa Mwanza.

"Maji ni huduma ambayo haina mbadala, serikali kwa kutambua hilo ikaamua kufanya uwekezaji wa kutafuta majawabu ya tatizo la maji safi na salama kwa wananchi wa Jiji la Mwanza na viunga vyake, na wameanza kupata maji tumetembelea, tumeona kazi imetekelezwa vizuri, " alisema Mzava.

**"Maji ni huduma ambayo haina mbadala, serikali kwa kutambua hilo ikaamua kufanya uwekezaji wa kutafuta majawabu ya tatizo la maji safi na salama kwa wananchi wa Jiji la Mwanza....**

Alisema kazi ya kutibu maji taka yanayozalishwa viwandani, nyumbani na maeneo mengine ya biashara lazima ifanyike kwa makini ili yasiendelee kuzagaa juu ya uso wa dunia, kuharibu mazingira na kusababisha matatizo ya afya kwa jamii.

Meneja Miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Celestine Mahubi, alisema mradi huo wa kuondoa na kutibu maji taka wanautekeleza kwa gharama ya Sh. bilioni 1.96 ili kulinda chanzo cha maji cha ziwa hilo.

Kuhusu mradi wa chanzo cha maji Butimba, alisema umegharimu Sh. bilioni 71.69 na kukamilika kwa asilimia 100.

Alisema chanzo hicho kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 48 za maji kwa siku na baadhi ya wananchi wameanza kunufaika.

# Mwassa aibua kiini lishe duni Kagera

**Na Restuta Damian,** KAGERA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwassa, amesema wakazi wa mkoani hapa hawana utamaduni wa matumizi sahihi ya vyakula wanavyozalisha na kusababisha kuwa miongoni mwa mikoa yenye tatizo la lishe duni nchini.

Mwassa alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yanayofanyika kitaifa mkoani hapa kuanzia Oktoba 10 hadi 16, mwaka huu.

Alisema Kagera unazalishwa ndizi, maharage, mahindi, karanga, mihogo, viazi vitamu na lishe kwa wingi, lakini tatizo ni matumizi kwa wakazi wake.

"Kinachofanya lishe kutokuwa vizuri ni pamoja na wananchi kutotumia vyakula hivyo kwa usahihi, kula milo isiyo kamili na kuuza mazao ili kujipatia kipato," alisema.

Kuhusu maadhimisho hayo, Mwassa alisema, mkoa umejipanga kushirikiana na Wizara ya Kilimo kufikisha maudhui kwa wananchi nchini na kuhimiza ulaji na kulima vyakula vinavyohitajika katika mwili wa binadamu.

Katibu Tawala Msaidizi Upande wa Uchumi na Uzalishaji wa mkoa huo, Isaya Tendega, alisema hali ya uzalishaji wa vyakula mkoani hapa bado ipo chini ikilinganishwa na mahitaji, hivyo kulazimu chakula kingine kutoka nje ya mkoa.

Pendega, alisema uzalishaji wa vyakula ndani ya mkoa ni tani milioni 3.4 na matumizi milioni 7.7 huku zaidi ya 2.7 zikiuzwa nje.

# Mbunge ajinasua kijiji kukosa huduma za afya

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKAZI wa Kijiji cha Mwasele wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga wamemtaka Mbunge wao wa Kishapu, Boniphace Butondo awaeleze sababu ya serikali kushindwa kujenga kituo cha afya katika maeneo.

Wakazi hao, akiwamo Said Hamis, wakizungumza juzi kwenye mkutano wa mbunge huyo uliofanyika Mji wa Mhunze, walidai kukosekana kwa kituo hicho kunasababisha maisha yao kuwa hatarini kwa watakaohitaji matibabu ya dharura baada ya kuugua ghafla.

Hamisi, alisema serikali imekuwa ikijenga vituo vya afya, zahanati na hospitali kwenye maeneo mengine na kukiruka kijiji chao, kitendo kilichowalazimu kumhoji mbunge wao ili kupata majibu. Akizungumza katika mkutano huo, Mbunge Butondo, aliuagiza uongozi wa kijiji hicho kushirikiana na diwani wa kata yao kutafuta eneo la kujenga zahanati. Aliahidi kutoa mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya hatua za awali za ujenzi na zahanati hiyo na kuwataka wakazi hao kumbana mkurugenzi wa halmashauri yao kukamilisha ukifika hatua ya renta.

# Wauziwa ndoo 1,000/- kwenye tingatinga

**Na Judith Julius,** NGARA

WAKAZI wa Kata ya Nyamiaga wilayani hapa Mkoa wa Kagera wamedai hawana huduma ya majisafi na salama katika maeneo yao tangu mwaka 1974.

Wakazi hao walitoa kilio hicho juzi katika mkutano wa Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoro, uliofanyika Kijiji cha Kumuyange.

Mmoja wa wakazi hao, Magreth Gwassa, alidai wamekuwa wakitumia maji yasiyosalama kwa afya zao ya kwenye tingatinga kwa kuuziwa ndoo kwa Sh.1,000 na kusababisha baadhi yao kukumbwa na magonjwa ya tumbo.

George Ngeze (66), alidai tangu kuzaliwa kwake ameshuhudia familia nyingi zikitumia maji yaliyopo kwenye tingatinga ambayo si salama kwa afya zao.

Diwani wa Kata hiyo, Eustasi Majita, alithibitisha kata hiyo kukosa maji safi na wakazi wake kutumia muda mwingi kusaka na kushindwa kushiriki katika shughuli zao za kiuchumi.


Akijibu kero hiyo, Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani hapa, Simon Ndyamkama, alisema wanajenga vyanzo viwili vya maji kwa ajili ya kusambaza maji safi na salama katika kata hiyo.

Ndyamkama, alivitaja vyanzo hivyo kuwa ni matangi mawili yenye ujazo wa lita 25,000 na 75,000 kwa gharama ya zaidi ya Sh.bilioni 1.6 ili kuwahudumia wakazi hao wakati wote.

Alisema mamlaka hiyo pia inatarajia kujenga mtandao wa maji na kutengeneza kituo cha kuchota maji kwa kadi ya malipo ya kabla kwa ajili ya wakazi hao.

Mbunge Ruhoro alimwagiza Meneja wa RUWASA kumsimamia mkandarasi ili akamilishe kwa wakati mradi huo ukutekeleza adhima ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani. "Mradi huu ukamilike ndani ya miezi sita kama ilivyopangwa kwani wananchi wameteseka kwa muda mrefu, wanahitaji kupata huduma hiyo muhimu," alisema.

Ukurasa 13




Miaka 25 bila Nyerere, tukumbuke kaulimbiu ajenda yake 'Mtu ni Afya'



**WANAFUNZI WASHINDI TUZO ZA YST... Wabuni ukuzaji kilimo maarufu cha mwani, huku wakinusuru uharibifu wa mazingira ya mikoko**

Ukurasa 12

BUFE
IJUMAA OKTOBA 11, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

ALIVYONADI NANENANE NA BARAZA LA BIASHARA...

# Rais ashuhudia shamba kubwa Ruvuma, ubunifu wa kuunganisha kilimo, biashara

• Amwelekeza Bashe, inafaa kuwa darasa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI anahutubia kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima - Nanenane yaliyofanyika katika Uwanja wa Nanenane Nzuguni, DodomaAgosti mwaka huu,

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akatamka serikali imejipanga kujenga uchumi jumuishi, unaowainua wananchi wote kuwawezesha wanufaike ipasavyo.

Dk. Samia akafafanua kuna hatua iliyotumika kuongeza bajeti ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ili zilete mageuzi makubwa, ambayo akashuhudia matokeo yake chanya, kwa ishara aliyokutana nayo alipokuwa ziarani mkoa wa Ruvuma.

Sasa ni zaidi ya wiki moja iliyopita, akiona makubwa yanaendelea katika shamba kubwa la kahawa lenye kilimo cha kisasa na tija kubwa, ikibeba viashiria vyote vya uwekezaji chanya kitaifa.

Rais akafafanua kinachofanyika sasa, ni kuongeza maeneo ya umwagiliaji, matumizi mbolea, uzalishaji na usambazaji mbegu bora shambani na kuimarisha huduma za ugani.

Kwa mujibu wa Dk. Samia, mtazamo uliopo hapo ni kuboresha miundombinu ya kuhudumia mifugo, pamoja na upatikanaji huduma za ugani, chanjo, majosho na masoko nchini.

Ni tamko alilolitoa wiki moja na nusu kabla ya Nanenane mwishoni mwa Julai, katika Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), akiagiza kunakuwapo mifumo ya



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokagua kahawa bora, katika moja ya mashamba makubwa ya mfano, mwezi uliopita huko Peramiho, mkoani Ruvuma. **PICHA: MAKTABA.**

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini iiliyoboreshwa, imeunganishwa na kusomana nchini ifikapo Desemba mwaka huu.

Anasema, dhamira iliyoko ni kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi kupitia mifumo ya kielektroniki, ikiongeza kasi na uwazi katika utendaji kazi, huku TBNC nayo ikitambulika kuwa jukwaa muhimu linalojadili mazingira ya biashara, uwekezaji na uchumi kwa ujumla nchini.

Kupitia mkutano huo wa TBNC, akasisitiza agizo lake kuhakikisha mifumo ya TEHAMA nchini inaboreshwa, inaunganishwa na kusomana ifikapo mwezi Desemba mwaka huu, kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi kielektroniki na kuongeza kasi na uwazi wa utendaji kazi.

**VIWANDA KILIMO**

Katika Maonyesho ya Nanenane, Rais Dk. Samia, akasema serikali inaendelea na ujenzi, pia ukarabati wa viwanda vya uchakataji mazao ya mifugo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uvuvi, ukuzaji viumbe maji, kutafuta masoko na utoaji mikopo yenye masharti nafuu kwa wavuvi na wafugaji.

Rais anasema lengo la kujenga uchumi jumuishi, ni kuongeza tija katika sekta za uzalishaji na kupunguza umaskini wa kipato kwa mwananchi mmoja mmoja kutumia sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, kutengeneza ajira.

Dk. Samia anafafanua dhima iliyoko ni kuhakikisha chakula kinapatikana nchini, pia kuwapo mchango katika pato la taifa na uchumi kwa ujumla, huku akisisitiza serikali inalenga kuongeza bajeti za utafiti, ndio maana maabara na vituo vya utafiti vimezinduliwa, kuwezesha nchi kufikia masoko ya kimataifa.

**SHAMBANI PERAMIHO**

Akiwa katika ukaguzi wa mashamba mkoani Ruvuma, Rais akawaasaa kutunza fedha pale wanapouza nafaka zao kwa bei nzuri, ili soko linaposhuka wawe na hifadhi ya kutosha, akiwaelezwa kuwa bei za masoko hazitabiriki, hivyo ni muhimu kwa wakulima kuwa makini na rasilimali fedha wanazochuma.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amesema tarehe 24 Septemba 2024 wakati wa mkutano wake katika shamba kubwa la kahawa lililowekezwa Peramiho, mkoani Ruvuma.

Ni moja ya mashamba 50 makubwa ya kahawa nchini, likiwa na ukubwa wa ekari 50,000, ikizalisha kahawa kwa kutumia mfumo wa umwagiliaji matone (drip irrigation) na kutajwa kutoa kati ya wastani

Inaendelea Uk 14

## BIASHARA

### WANAFUNZI WASHINDI TUZO ZA YST...

# Wabuni ukuzaji kilimo maarufu cha mwani, huku wakinusuru uharibifu wa mazingira ya mikoko

1.



Wananfunzi washindi wa tuzo ya jumla ya YST, Rasasha Amin Hamis na Ramra Tamad Abdullah, Zanzibar walipokabidhiwa zawadi zao. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

**Na Elizabeth Zaya**

RASASHA Amin Hamis na Ramra Tamad Abdullah ni wanafunzi wa kike wanaosoma katika Shule ya Sekondari Lumumba, iliyoko visiwani Unguja.

Wanafunzi hao mwaka huu wameibuka washindi wa jumla katika tuzo za Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST), baada ya kubuni mradi wa kutumia mbinu mbadala inayohifadhi mazingira na kuokoa ukataji wa misitu katika kilimo cha mwani.

Kwa mujibu wa wanafunzi hao watafiti, asilimia kubwa ya wakulima wa zao la mwani visiwani Zanzibar hukata miti hasa mikoko, ambayo wanatengenezea vijiti vinavyotumika kwenye kilimo hicho.

"Mradi wetu ulihusu utumiaji wa matumbawe katika kilimo cha mwani, ambayo tuliichagua kwa sababu kwa Tanzania hasa Zanzibar. Tuna watu wengi wanaojishughulisha na kilimo cha zao hilo, lakini namna wanavyokiendesha, wanahusisha ukataji wa misitu hasa mikoko ambavyo wanatengeneza vijiti ambavyo wanavitumia katika kilimo hicho cha Mwani," anasema Ramra na kuiongeza:

"Licha ya kwamba tunaamini kuwa kilimo hicho cha mwani ni kizuri na muhimu, lakini kinachangia uharibifu wa misitu na mazingira hasa mikoko ambapo baada ya kutafiti tulibaini kwamba takribani misitu 400,000 inakatwa kila mwaka kwa ajili ya matumizi ya kilimo cha zao hilo."

Anasimulia kwamba, kwa kubaini uharibifu huo wa mazingira, ndipo wakapata wazo la kuja na mradi unaonusuru mazingira na wakati huohuo, inakomboa kilimo.

"Tukafikiria kwamba miaka ijayo kama wakulima wa mwani wataendelea kukata mikoko namna hiyo, yote itapotea na hali huenda ikazidi kuwa mbaya zaidi kwa miaka 10 au 20 ijayo.

"Hivyo tukaona tutafute majibu au njia ambayo itakuwa mbadala wake kwamba badala ya kutumia au kukata mikoko kwa ajili ya kutengeneza hivyo vijiti, tukaona inawezekana kutumia Matumbawe," anasema Ramra.

"Baada ya kupata hilo wazo, tulienda tukafanya utafiti wa Matumbawe, tukaona kwamba yenyewe yatasaidia katika matumizi ya kilimo hicho cha mwani, kwa sababu yanatoa virutubisho ambavyo vinahitajika katika upandaji zao hilo na tukabaini kwamba yenyewe ina uwezo wa kuruhusu viumbe vingine viishi kama samaki na viumbe wengine.

"Pia, tulibaini kwamba matumbawe pamoja na mwani yana uwezo wa kufyonza cabondioxide kwa hiyo tukaona itasaidia kupunguza kiwango cha hewa hiyo, tukaona ndio njia sahihi ya kutumia," anaeleza.

Kadhalika, anataja kutumia Matumbawe, kupitia utafiti waliofanya katika vijiji vinne vinavyolima sana zao hilo la mwani, upo uwezekano wa kuvuna mwani mwingi zaidi na kwa muda mfupi tofauti na ilivyo kwa kutumia vijiti vya miti kama ambavyo wamekuwa wakifanya siku zote.

"Kwa hiyo njia yetu sisi ilihusisha utumiaji matumbawe katika kukuza mwani badala ya kutumia vijiti na kwa kuwa tulikuwa na miezi mitatu tu ya kufanya mradi, badala ya kutumia Matumbawe.

"Tulitumia mawe ambayo yana sifa sawa na hayo na hivyo tukagundua kwamba kwa kutumia mawe hayo. Mwani unaweza kukua kwa haraka na tukakuza pia samaki kwa wakati mmoja," anasema Ramra.

Anaendelea: "Na kwa kutumia njia hiyo, tukatunza mazingira, tukavuna mwani mwingi na tukavuna pia samaki. Kwa hiyo, tunajikuta tunapata faida nyingi zaidi, tena kwa muda mfupi.

"Kwa hiyo endapo tungetumia njia wanayotumia wakulima kwa sasa, tungekata misitu tukaharibu mazingira, tunatumia muda mwingi mpaka kuvuna lakini hata wakati wa mavuno unapofika, tunavuna kidogo.

"Tukagundua kwamba njia ya kutumia matumbawe ni bora zaidi kwa sababu mbali na kutunza mazingira lakini faida za kiuchumi ni kubwa zaidi."

**USHAURI KWA KILIMO**

Wanafunzi hao wanaishauri serikali iangalie namna ya kutoa elimu kwa wakulima wa zao hilo, ili watumie njia nzuri ya kulima ambayo haitaendelea kuharibu misitu na mazingira.

Wanasema endapo wakulima wataendelea kutumia njia hiyo ya kukata miti katika zao hilo la Mwani, hali ya mazingira itazidi kuwa mbaya na kwamba njia mbadala isiyoharibu mazingira, ndio itasaidia kuimarisha uchumi wa buluu.

"Kama sisi tumefanya utafiti na tukabaini kwamba kwa kutumia njia mbadala inawezekana tukaokoa misitu yetu, hatuoni haja ya kuendelea kulima kwa kukariri au mazoe kwa sababu ni hatari kwa vizazi vijavyo," anasema Ramra.

Ikumbukwe kwamba, mashindano hayo ya YST, mwaka huu yamefanyika kwa mara ya 14 na hufanyika kila mwaka kwa kushirikisha wanafunzi wanasayansi kutoka katika shule mbalimbali za sekondari Tanzania Bara na Zanzibar.

**YALIVYO MASHINDANO**

Mashindano hayo ambayo huambatana na maonesho ya kazi za kibunifu za kisayansi, huanza kushindanisha kazi za kibunifu za kisayansi za wanafunzi hao kuanzia katika mikoa mbalimbali lakini pia huwa inafanyika fainali ambayo hushindanisha kazi bora zaidi ambazo hupatikana baada ya mchuJo kutoka katika maonyesho ya kazi hizo yanayofanyika mkoani.

Fainali za mashindano hayo kufanyika baada ya kupatikana kazi bora zaidi na miaka yote hiyo, yamekuwa yakihitimishwa jijini Dar es Salaam na mwaka huu imefanyika Septemba katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNICC), washindi katika makundi mbalimbali hupata tuzo za medali, fedha taslimu pamoja na ufadhili wa masomo wa chuo kikuu.

Washindi wanne pekee ndio hubahatika kupata ufadhili wa masomo ya vyuo vikuu, wawili wakiwa washindi wa jumla na wawili wengine ni wale wanaobahatika kushinda katika kategoria maalumu ya Karimjee Jivanjee Foundation ambao ndio wadhamini wakuu wa mashindano hayo ya YST kwa miaka 14 mfululizo.

Washindi wengine kutoka katika kategoria mbalimbali hushinda medali pamoja na fedha tasilimu.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi ya YST, Prof. Yunus Mgaya, washindi hao wa jumla walipatikana baada ya kufanyiwa mchujo ulioshirikisha kazi 1,055 kutoka kwa wanafunzi wa sekondari wa mikoa mbalimbali ya pande zote za muungano.

Prof. Mgaya anasema gunduzi za mwaka huu, zilijikita katika masuala mbalimbali, ikiwamo uhifadhi salama wa mazao ya kilimo, afya ya binadamu, mifumo ya umwagiliaji, utunzaji wa mazingira, upatikanaji wa nishati ya umeme, usalama wa chakula na utatuzi wa changamoto kidijitali.

Mwazilishi mwenza wa YST, Dk.Gozbert Kamugisha, anasema kupitia tuzo hizo, wameanza kuona tija yake hasa katika kutengeneza wabunifu na wanasayansi wengi nchini na pia kuwahamasisha wanafunzi kupendelea masomo ya sayansi.

Anasema baadhi ya wanafunzi waliowahi kupata tuzo tangu zianzishwe miaka 14 iliyopita, tayari wengine ni madaktari wazuri, wahandisi na wanateknolojia wa kubuni mambo mbalimbali.

•



Kilivyo kilimo cha mwani, Zanzibar**. PICHA: MAKTABA**

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Miaka 25 bila Nyerere, tukumbuke kaulimbiu ajenda yake 'Mtu ni Afya'







**NA SABATO KASIKA**

JUMATATU ijayo itakuwa inatimia miaka 25 tangu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kufariki dunia. Baba wa Taifa ambaye ni Rais wa kwanza wa Tanzania, alifariki dunia Oktoba 14, mwaka 1999.

Pamoja na kwamba zimebaki siku tatu kutumia miaka 25 tangu afariki dunia, lakini ukisikiliza hotuba zake kupitia runinga na redio, misemo au maandiko yake unapata hisia bado vinaishi.

Tunapoelekea kwenye kilele cha maadhimisho ya kifo cha kiongozi huyo aliyeifanyia mengi nchi hii, kwa manufaa ya Watanzania, ni vyema tukumbushane baadhi ya yale aliofanya, hasa kwa upande wa afya.

Katika jitihada za serikali yake za kuimarisha afya na kuhamasisha wananchi kujikinga na adui maradhi, alikuja na kaulimbiu ya 'Mtu ni Afya' alioanzisha mwaka 1973 hadi mwishoni mwa miaka hiyo ya 70.

Nakumbuka kaulimbiu hiyo kwani ilikuwa ni kielelezo kuhusu afya mazingira, kutokana na ukweli kwamba serikali yake ilithamini afya, huku ikihamasisha usemi wa 'Kinga ni Bora Kuliko Tiba.

Kimsingi ni kwamba, 'Mtu ni Afya', ni kaulimbiu iliyolenga kutoa ujumbe maalum kwa jamii, kwamba bila ya kuwa na mazingira bora, binadamu hawezi kupata afya nzuri, kwani anaweza kuwa mwathirika maradhi yote hatari.

Wale ambao tayari walikuwa wameshajitambua kiumri wakati huo, watakuwa wanakumbuka jinsi ambavyo kaulimbiu ya 'Mtu ni Afya' ilivyokuwa ikisikika redioni na kutangazwa pia magazetini na hata katika mbalimbali, ikiwamo ya mikutano ya hadhara.

Lakini, pia ilifikia hata bendi ya muziki wa dansi nazo zikaitungia nyimbo kaulimbiu hiyo kwa ajili ya kusaidiana na serikali, katika kuhamasisha umuhimu wa kila Mtanzania kuwa na afya bora.

Ninaamini kwamba, Watanzania waliokuwapo wakati huo ambao hadi sasa wapo, watakuwa jinsi ambavyo Mwalimu Nyerere alihimiza umuhimu wa afya bora inayotokana na lishe bora.

Hivyo, tunapoadhimisha miaka 25 ya kifo chake, nimeona tukumbushane machache aliofanya kwenye afya wakati wa uongozi wake, hasa kwa kuzingatia kwamba alikuwa hampendi adui maradhi.

Ikumbukwe kuwa baadhi ya nchi kupata uhuru, Mwalimu Nyerere alitangaza vita dhidi ya maadui watatu ambao ujinga, umaskini na maradhi, ambayo alipambana nayo kwa nguvu zake zote.

Njia kuu aliyotumia kupambana na adui maradhi, ni kuwapa elimu Watanzania ili waweze kutambua mbinu mbalimbali za kujikinga au kutibu maradhi kwa kwenda hospitali kupata huduma za afya.

Bahati nzuri ni kwamba, hata baada ya yeye kung'atuka, awamu zilizofuata, zinaendeleza yale ambayo alianzisha ikiwamo mkakati unaoendelea sasa wa kujenga zahati kila kijiji.

Mkakati huo unakwenda sambamba na ujenzi wa vituo vya afya kila kata, hospitali za wilaya, za mkoa na za rufani, ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kutimiza kaulimbiu kwa ajili ya 'Mtu ni Afya'.

Kaulimbiu 'Mtu ni Afya', pia inahimizwa kwa njia ya kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, rufani na taifa, kwani bila kuwa na afya bora, si rahisi mtu kuweza kushiriki katika shughuli za maendeleo yake binafsi na hata ya taifa.

Hatua hiyo haishii hapo tu, bali pia matangazo mbalimbali yanayohusu afya au kijinga na maradhi yakiwamo ya milipuko kama kipundupindu, kuhara na mengine, huwa yanaandikwa kwenye magazeti.

Vilevile, huwa yanasikika redioni, katika runinga na mitandao ya kijamii, ili kufikisha ujumbe kwa Watanzania ili wawe tayari linapotokea tatizo, wajue jinsi ya kuchukua tahadhari.

UCHUMI

# Wenye shida ya kuona 25 katika kijiji kimoja wanavyopambana na uchumi

## •Kila Jumatatu wakutana kujadili maisha yao

**Na Mwansdishi Wetu**

MOSES Mugabe (53) anaishi Mashariki mwa Uganda. Hajui ni nini kilichomfanya apoteze uwezo wa kuona, ila anakumbuka mara ya mwisho kuona jua likichomoza, kumbukumbu anayoienzi.

"Niliishi maisha ya kuhuzunisha baada ya kupata habari kwamba nimepoteza uwezo wangu wa kuona kabisa na kwamba sitawahi kuona tena maishani," anasema.

Moses ni miongoni mwa raia milioni tatu nchini Uganda walio na matatizo ya kuona, kulingana na takwimu kutoka Shirika la Kimataifa la Kudhibiti Upofu (IAPB)

Kote barani Afrika, kuna watu milioni 100 wasioona. Kwa raia wengi wa Uganda wanaoishi mijini wanapata matibabu, wwanaoishi maeneo vijijini bado hawapati huduma stahiki kwa afya ya macho, huku Uganda ikitajwa kuwa na wataalamu wachache wa macho.

Bila matibabu wengi kama Moses wametafuta mbadala wa kuishi bila kuona. Yuo na familia, mke na watoto wao watatu katika kijiji cha Luubu, kilichoko kwenye jirani na Ziwa Victoria.

Luubu ilikuwa shule iliyojengwa katika miaka ya 2000 kwa ajili ya watoto waliokuwa na matatizo ya kuona. Moses anaongoza kikundi cha jamii ya wasioona huko Luubu, ambako kuna jamii ya watu 25 wasioona.

Wanaishi katika eneo moja na wote wanatumia vyoo viwili vya Pamoja, wakiwa na kawaida ya kukutana kila Jumatatu chini ya mti mkubwa wa mfenesi, kujadili changamoto wanazopitia.

Moses, anayejulikana kwa heshima ya Mwenyekiti, huongoza mkutano, mmoja wao akisikika kutamka: "Tunaomba misaada ya vifaa vya kutusaidia kusikia zaidi."

Mwingine anapaza sauti kuhusu ongezeko la karo ya shule, huku Moses akmjibu kwa utulivu, kwamba: "Msikubali kudhulumiwa haki zetu kwa vile sisi ni walemavu, tutazungumza ili kila mmoja ajue thamani yetu."

Mikutano hiyo ya kila wiki imekuwa na umuhimu mkubwa, Mwenyekiti Moses, akawa na ufafanuzi kwamba wanazungumzia "jinsi ya kusaidiana na kuwasomesha watoto wao, jinsi ya kuwalisha watoto wetu, kuwavisha na vile tutakavyopata huduma bora za matibabu."



Baadhi ya wakazi wa kijiji kilichoko Uganda, wengi hawaoni. **PICHA: MTANDAO.**

### WASIOONA UGANDA

Inatajwa, huenda wakazi wa Luubu wamepoteza uwezo wa kuona kwa sababu kadhaa, kama vile 'homa ya mto' au 'onchocerciasis', kisukari, ukambi, ugonjwa wa mtoto wa jicho na trachoma.'

Inatajwa kuwa watu wengi kama Moses, hawajawahi kuelezwa hali zao na daktari, ikirejewa katika miaka ya 1990 hadi 2000, ugonjwa wa 'homa ya mto' unaosababisha upofu ulienea kote Mashariki mwa Uganda na hasa katika wilaya ya Mayuge.

Ni ugonjwa unaosababishwa na minyoo wa majini na kusambazwa kwa binadamu kupitia kuumwa na nzi weusi wanaobeba ugonjwa huo; makazi yaliyoko kwenye ufuo wa Ziwa kama Luubu yaliathirika zaidi.

Hata hivyo mwaka wa 2017, baada ya kuzinduliwa kwa miradi ya kupambana na homa hiyo, homa ya mto iliisha katika Wilaya ya Mayuge.

Huenda ugonjwa huo haupo kama zamani, lakini kijiji hicho cha wasiona cha Luubu kingalipo, Moses akitamka: "Kama jeshi kambini, tunaishi pamoja ili iwe rahisi kuungana kunapokuwa na jambo."

### SHIDA YA HUDUMA

Kunatajwa zaaidi ya watu milioni tatu nchini Uganda hawaoni na Waiswa Julius, ndiye daktari pekee anayehudumia kaunti ya Bukatebe kunakopatikana kijiji cha Luubu.

Yeye anasema huwa anafanya kazi mara mbili kwa wiki katika Kituo cha aAya cha Mayuge, akiwahudumia wakazi wa Luubu mara kwa mara.

Anasema kwamba umasikini na mazingira machafu ni baadhi ya sababu za idadi kubwa ya watu kupoteza uwezo wa kuona, miongoni mwa wakazi katika eneo hilo.

Pia, anatajai dhana za utamaduni, zinazowasukuma watu kutafuta dawa za kienyeji pia zinachangia pakubwa.

Dk. Julius anasema, imani hizo zinaweza kuwazuia watu kutafuta huduma za matibabu wanazohitaji na huwaona madaktari wakati wamechelewa mno.

"Kama serikali inaweza kuongeza idadi ya wataalamu wa macho kwa kila wilaya, nadhani itakuwa bora," anasema Dk. Julius.

Mtaalamu wa Magonjwa Ambukizi katika Wizara ya Afya nchini Uganda, Dk. Alfred Mubangizi, anasema serikali inatoa udhamini wa masomo ya madaktari wachanga ili wawe wataalamu wa macho.

"Tunawafunza madaktari. Serikali inawahimiza kusomea shahada za uzamili katika somo la utaalamu wa macho ili tupate madaktari wengi zaidi,"

### NGUVU YAO ULEMAVU

"Kile tulichojifunza mwanzo ni umoja. Kila mtu anamhitaji mwenzake na ulemavu wetu ndiyo nguvu yetu," anasema Moses.

Anataja changamoto tatu zinazoikumba jamii hiyo, ni kuepuka unyanyapaa, kukosa urithi katika familia zao na kupata mchumba.

Jamii yake pia inatia bidii kuwaelimisha watoto wao ambao pia hawaoni vizuri ama waliopofuka, ikimaanisha kuwapeleka katika shule za bweni zilizoko mbali na nyumbani.

Moses ana matumaini kwamba wanawe watafuzu kwa shahada za uzamili na za uzamifu. Katika kufaulu hivyo, anasema watasaidia kuondoa unyanyapaa na kuipa jamii hii kesho iliyo bora.

"Watakapokuwa wameelimika vya kutosha, hakuna atakayewaona kama vipofu. Watu wataangalia mafanikio yao badala ya kuwatenga," anasema.

"Tutazungumzia haki zetu katika kila fursa tutakayopata, haijalishi lolote, sauti zetu zitasikika na wito wetu kujibiwa."

• ***Kwa mujibu wa BBC.***

# RAIS ASHUHUDIA SHAMBA KUBWA RUVUMA, UBUNIFU WA KUUNGANISHA KILIMO, BIASHARA

Inatoka Uk 11

wa asilimia nne hadi tano ya kahawa aina ya Arabica, inayozalishwa nchini.

"Mwekezaji huyu amekuwa akitushika mkono katika maeneo ya elimu, afya na hata uzalishaji wa miche. Sasa ni kwenda kuongeza tija kwenye uzalishaji wa jamii kwa kuchimba visima kwenye mashamba ya wakulima wadogo wa kahawa wa pembezoni mwa shamba hili...," anatamka Rais alipozuru shambani hapo.

Anaongeza, kwa kufanya hivyo kunatoa manufaa ya kuhamisha ujuzi kwa wakulima, ili kuwa na kilimo cha kisasa cha umwagilaiji.

Rais Dk. Samia, pia hakuficha furaha yake kupitia ushuhuda wa kubuni mazao mengine mahali hapo, kama vile pilipili manga na 'paprika' au pilipili hoho nyekundu iliyosagwa, ambayo tayari kuna soko kubwa kwenye nchi za bara la Asia.

"Kwa kuwafundisha wakulima hawa wadogo wa pembezoni jinsi ya kulima kisasa na kuhifadhi mazao haya ya kahawa, pilipili manga na 'paprika', linakuwa soko la uhakika," akatamka Rais, ambayo kupitia hadhira hiyo akatoa maelekezo kwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kuhusu cha kufanya.

Mtazamo wa kwanza, unahusu kuwa mbegu za kahawa zinazoenda kwa wakulima, ziendane na mradi huo, hususan kwa vile serikali imeanza kutoa ruzuku kwa mbegu za kahawa.

Mkuu wa Nchi pia akaongeza kuwa ni hali inayosaidia kuongeza tija kwenye kilimo cha kahawa, ambacho uzalishaji wake kwa sasa ni tani 65,000 kwa matarajio ya mauzo ya Dola za Marekani Milioni 150 hadi zaidi 250. Matarajio mapya ni hadi kufika zaidi ya tani 80,000.

Waziri Bashe, pia ameelekezwa kuhakikisha minada ya uuzaji kahawa iwe ya uwazi, ili wakulima wanufaike moja kwa moja huku wakipokea malipo yao ndani ya siku mbili hadi tatu.

Kuhusu Vyama vya Ushirika, akaeelekeza kuwa vizidi kuwa imara na kuondokana na makato ya kinyemela na ujanja, kuhakikisha kuna mifumo inayoeleweka kwa maslahi ya wakulima.



# EWURA yafungua milango malalamiko maji, umeme, mafuta

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetoa wito kwa wananchi kuwasilisha malalamiko kwa kukosa huduma bora ili yapatiwe ufumbuzi.

Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa EWURA, Tobietha Makafu, alitoa wito huo jana jijini hapa wakati akielezea Mamlaka hiyo ilivyojipanga kuwahudumia wadau wake katika Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyoanza Oktoba 7, mwaka huu.

Makafu alisema kuwa; "Mathalani mtu amejenga nyumba yake, amelipia huduma ya kuunganishiwa umeme au maji, lakini unapita muda mrefu bila kupata huduma hiyo, tunakusihi leta malalamiko hayo kwetu na sisi EWURA tutahakikisha unapata huduma hiyo kwa mujibu wa utaratibu uliopo kisheria," alisema.

Vilevile, alisema mteja anapopelekewa ankara ya maji kama hajaridhiki nayo, au msoma mita anakadiria bila kusoma mita, mteja anapaswa kuwasilisha suala hilo kwa mamlaka ya maji na kwamba kama hakupata atoe taarifa EWURA.

"Sisi tutahakikisha tunamsaidia kupata mustakabali wa suala hilo," alisisitiza Makafu.

> **"Bidhaa ya mafuta inatoka haraka hivyo ni muhimu kuwasiliana nasi kwa haraka kabla mafuta yanayohusika haijaisha ili wataalamu wa EWURA waweze kufanya uchunguzi...**

Kuhusu malalamiko kuhusu mafuta, alisema inapotokea mteja ameweka yakasababisha chombo kuharibika, anapaswa kuwasilisha kwa msimamizi wa kituo cha mafuta na endapo hatapata ufumbuzi EWURA ndani ya siku saba ili yashughulikiwe.

"Bidhaa ya mafuta inatoka haraka hivyo ni muhimu kuwasiliana nasi kwa haraka kabla mafuta yanayohusika haijaisha ili wataalamu wa EWURA waweze kufanya uchunguzi na kumwezesha mteja kupata haki yake," alisema Makafu.

Kuhusu wiki hiyo, alisema katika Ofisi ya Makuu Makuu ya EWURA, wateja wamepata fursa ya kuhudumiwa moja kwa moja na Mkurugenzi Mkuu, Dk. James Andilile na Wakurugenzi wa Idara na kwa Ofisi za Kanda, watendaji wametoka ofisini kuwafuta wadau wao.

"Mathalani Kanda ya Magharibi, wanatoa huduma katika viwanja vya shule ya msingi Uyui mkoani Tabora, hivyo tumejipanga kuhakikisha kila mwenye changamoto anapata huduma," alisema.

Alisema wamejipanga kuhakikisha kila mwananchi anaendelea kupata huduma bora za umeme, mafuta, gesi asilia, maji na usafi wa mazingira.



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bestina Magutu, wakati wa maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima katika viwanja vya Chipukizi, mjini Tabora jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# AAFP yashauri vyama kuteua wagombea wanaokubalika

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

CHAMA cha Wakulima (AAFP) kimevishauri vyama vya siasa nchini kuteua wagombea wanaokubalika kwa wananchi ili wawachague katika chaguzi zijazo na wawaletee maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Chama hicho Taifa, Mark Mhemella, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzingatiaji demokrasia unaofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kuelekea kwenye uchaguzi huo wa wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji.

Alisema chama hicho kimetoa ushauri huo ili kuondokana na mtindo wa baadhi ya vyama kupenyeza majina ya watu wanaowataka ili wagombea na kushinda kwa maslahi binafsi, hivyo kushindwa kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema chama hicho kinatarajia kuona uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na mkuu mwakani utakuwa wa haki na huru kwa vyama vitakavyowateua wagombea wanaokubalika kwa wananchi ili kuendana na falsafa ya Rais ya R4.

"Tunampongeza Rais kwa kusimamia demokrasia nchini, hii itawapa nafasi kubwa wananchi kuwachague viongozi wanaowataka wenyewe kupitia falsafa ya R4, pia tunawaka viongozi wetu kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, kata, vijiji hata mitaa kushiriki ipasavyo kwenye uchaguzi huu ili kupata idadi kubwa ya uwakilishi katika maeneo mbalimbali," alisema huku akitumia fursa hiyo kutangaza mpango wa chama hicho kushiriki katika uchaguzi huo mitaa na vijiji unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Chama hicho Wilaya ya Dodoma, Exsavery Mapunda, aliwaomba viongozi wa siasa kuacha tabia ya kuchagua watu wanaowataka kuwaweka madarakani badala ya wale wanaopendekezwa na wananchi.

Mapunda, alisema baadhi ya viongozi waliopewa dhamana ya kupitisha majina ya wagombea wamekuwa na utashi wa kuwachagua wanaowataka ili kulinda maslahi yao.

"Tabia hiyo ya viongozi ya kujipangia safu zao za uongozi tofauti na wanaowataka wananchi kuna hatari ya Taifa kukosa wabunge, madiwani na wenye viti wa mitaa na vijiji wazalendo," alisema.

Mwenyekiti huyo, alisisitiza kuwa tabia hiyo itawakatisha tamaa wananchi kuvipenda vyama vyao na kutoshiriki katika chaguzi nchini, hivyo kukosa viongozi watakaowaletea maendeleo.

# Wanachama wakumbushwa kuhakiki michango NSSF

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WANACHAMA wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wametakiwa kujenga utamaduni wa kufuatilia na kuhakiki taarifa za michango yao mara kwa mara wakiwa kazini badala ya kusubiri kustaafu.

Meneja wa NSSF Mkoa wa Singida, Oscar Kalimilwa, alitoa rai hiyo juzi wakati ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja mwaka huu mkoani hapa.

"Tunatambua mchango mkubwa wa wateja wetu katika kuwezesha mfuko wetu kuendelea kufanya shughuli zake kuu nne," alisema na kuzitaja kuwa ni uandikishaji wanachama, ukusanyaji michango, ulipaji mafao na uwekezaji na kuwaomba wanachama wao kuhakiki michango yao mara kwa mara.

Kalimilwa, alisema mfuko huo hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha uliopita wa 2023/24 ulikuwa na wanachama 1,354,985 na waajiri 43,430 na kuandikisha wanachama wapya 291,266.

Alisema kwa mwaka 2024/2025 wamelenga kuandikisha wanachama wapya 324,321 na kwamba mfuko umekamilisha taratibu zote za uanzishwaji wa mfumo wa ufunguzi na malipo ya mafao kupitia mtandao kwa kuanza baadhi ya mikoa.

"Huduma hii inatoa fursa kwa wanachama waliopo mbali na matawi yetu kuweza kufungua matawi mahali popote walipo, kufuatilia maendeleo ya ulipaji na hatimaye kulipwa kwa mujibu wa kanuni za ulipaji wa mafao," alisema.

Aliongeza kuwa wajibu wa watumishi mfuko huko ni kuhakikisha wanafikia matarajio ya wateja na wadau wao ikiwa ni pamoja na wastaafu wanaopokea mafao, wanachama waliopo sasa na baadaye.

Kalimilwa alisema mfuko umeboresha mfumo wa sekta isiyo rasmi mahususi kwa wanachama wote walioajiriwa na umeandaa skimu kwa wafanyakazi katika sekta rasmi ili kujichangia kwa hiari kupitia skimu hiyo.

Alisema skimu hizo, NISS na SS zinalenga kupanua wogo wa huduma za hifadhi ya jamii nchini na kuchangia kuondoa umaskini kwa wananchi.

Ofisa NSSF Mkoa wa Singida, Kenneth Kalinjuma, alisema mfuko huo umepanua wigo wa hifadhi ya jamii kwa kuyafikia makundi yote ya wananchi waliojiajiri wakiwamo waendesha bodaboda, bajaj, mama na baba lishe, wakulima na wafugaji ambao wanafika kujiandikisha kwa ajili ya kuweka akiba zao ambazo zitawasaidia baadaye.

Wiki hiyo ilianzishwa kimataifa mwaka 1987 kwa lengo la kutambua umuhimu wa huduma bora kwa wateja na juhudi za wafanyakazi wanaotoa huduma bora kwa wateja.



# WAVIU: TARURA imeboresha maisha yetu

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WATU wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) wilayani hapa Mkoa Njombe, wameushukuru Wakala wa Barabara wa Mijini na Vijijini (TARURA) kwa kuwapa zabuni za ujenzi wa miradi na kuboresha maisha yao kutokana na kipato.

Hayo waliyasema juzi mbele ya viongozi wa Wizara ya Miundombinu kutoka nchini Sierra Leone baada ya kumbelea vikundi viwili, kikiwamo Tujipime kwa lengo la kujifunza jamii inavyoweza kushirikishwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Walisema zabuni hizo zimewawezesha wanachama wa kikundi hicho kuinua hali ya maisha yao, uchumi, maendeleo kwa kujenga nyumba na kununua mashamba na viwanja.

Mmoja wa wanachama wa Tujipime, Aulelia Theodori, alisema miradi hiyo pia imewasaidia kupata fedha za kusomesha watoto wao kuanzia elimu ya msingi hadi chuo kikuu.

"Kwa kweli tunafarijika tupo pamoja tunafanya kazi, tumejenga nyumba tumenunua mashamba, viwanja mpaka sasa hatujapata changamoto yoyote na tumefanikiwa kuwa na vikundi vya kukopeshana na kusaidiana katika shida na raha," alisema Theodori.

Mwenyekiti wa Kikundi hicho, Melsela Mlelwa, alisema wanaishukuru TARURA kwa kuwasaidia kupata kazi kwa wakati na bila ya usumbufu wowote.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga alisema anajivunia kuwa na jamii iliyoweza kutengeneza umoja na kutambua fursa zilizoko.

"Kama hapa tumeona madaraja yalivyojengwa kwa ubora kwa kushirikiana na TARURA, hivi ni vikundi tu ambavyo vimeweza kupewa mafunzo ikiwa ni njia nzuri ya serikali kurudisha kwa jamii na jamii imedhihirisha kuwa inaweza kunusa na kuzitambua fursa zilizoko," alisema Kamonga.

**"Wilaya yetu imeweza kupokea ugeni kutoka wizara ya miundombinu waliokuja kujifunza namna ya ushirikishwa wa jamii katika miradi ya maendeleo huwezi ukaigilizia kwa mtu anayepata**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Olivanus Thomas, alisifu ujio wa wageni hao kwa ajili ya kujifunza ushirikishwaji wa jamii katika miradi ya maendeleo.

"Wilaya yetu imeweza kupokea ugeni kutoka wizara ya miundombinu waliokuja kujifunza namna ya ushirikishwa wa jamii katika miradi ya maendeleo huwezi ukaigilizia kwa mtu anayepata sifuri ndio maana ujio wa wageni wetu una maana yakuwa kuna kitu wamekiona katika ardhi ya Tanzania hususani Ludewa ndio maana leo hii tuko nao hapa wakijifunza," alisema Thomas.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Matengenezo ya Barabara kutoka Sierra Leone, Mohamed Kallon, alisema amefurahishwa na wakala huyo kuwa na mpango shirikishi wa vikundi vya jamii kwenye miradi ya barabara.

"Nimevutiwa na jitihada za kikundi cha wanaoishi na virusi vya Ukimwi ambao licha ya kufanya kazi za kuboresha barabara vijijini, nimependa kusikia mnashughuli nyingine kama ufugaji, kilimo na kukopeshana fedha," alisema Kallon.

Meneja wa TARURA Ludewa, Mhandisi Butene Jilala, alisema kuna vikundi 52 vya nguvu kazi vinavyotumia teknolojia na kimojawapo kinaitwa 'Tujipime' ni kikundi ambacho tumeanza kufanya nacho kazi mwaka 2020.

Tujipime chenye wanachama 22 wanaoishi na VVU kilisajiliwa mwaka 2019 na kuanza rasmi kazi 2020 za miradi ya TARURA Ludewa.

# Wakulima wahaha kusaka soko la mazao

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa Kata ya Kitandililo Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani hapa Mkoa wa Njombe, wameiomba serikali kutafuta soko la uhakika la mazao hususan mahindi ili wauze kwa tija na kuongeza kipato.

Ombi hilo walilitoa juzi wakati wakizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa msimu mpya wa kilimo wa mwaka 2024/2025 uliofanyika mjini hapa.

Walisema kwa sasa mazao hayo hususani ya mahindi hailingani na gharama za uzalishaji kwa kuuza debe lenye ujazo wa kilo 20 kwa shilingi 6, 000.

Mmoja wa wakulima hao, Erasto Ndulundu, aliiomba serikali kuhakikisha wadau wa pembejeo za kilimo hasa mbegu na mbolea wanafikisha vijijini na kuwaondolea gharama kubwa kufuata mjini.

Veronica Tweve, alisema wanatumia gharama kubwa katika kilimo na kwamba kwa kukosa soko la uhakika, wanalazimika kuuza mazao yao kwa hasara.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Peter Muro, alisema ili kuhakikisha wakulima wanapata tija, wataalamu wameanza kupima afya ya udongo bure na kuwataka wakulima kuhuisha taarifa zao kwa lengo la kupata mbolea za ruzuku.

Diwani wa Kata ya Kitandililo, Imani Fute, aliwataka wakulima kuachana na kilimo cha mazoea na kupata elimu kwa wataalamu wa kilimo.

Fute, aliwataka mawakala kuacha tabia ya kuwazuia wakulima pembejeo zisizo na ubora ili wapate mazao ya kutosha.

Baadhi ya wadau wa kilimo, akiwamo Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya One Acre Fund ya Njombe, Braiton Willa, alisema watahakikisha wanafikisha pembejeo hizo kwa wakati vijijini ili wakulima wapate kwa gharama nafuu.



Mafundi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Mara, wakishusha baadhi ya mabomba ili kuyatandaza katika vijiji vya Wilaya ya Musoma Vijijini, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wahamasishwa kujiandikisha daftari mpigakura

**Na Eizabeth John,** LUDEWA

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwenye daftari la mpigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa ili wapate sifa ya kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo kwenye maeneo yao.

Mtaka aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Mundindi wilayani hapa.

Mtaka alisisitiza kuwa ili kila mwananchi aweze kupata fursa ya kupiga kura ni lazima ajiandikishe kwenye daftari hilo.

"Wananchi hakikisheni mnajiandikisha kwenye daftari la wapigakura kuanzia oktoba 11 hadi 20, mwaka huu, vyama vya siasa tuleteeni wagombea wazuri kwa sababu serikali tutasimamia uchaguzi wa huru na haki," alisema.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa mkoa huo, Julius Peter, alisema ili mwananchi apate fursa ya kupiga kura ni lazima ajiandikishe kwenye daftari hilo. "Rai yangu wananchi wa Mundindi kwa umoja wetu tujitokeze kwa wingi, twende tukajiandikishe kwenye daftari hilo na uchaguzi kwa maana uchaguzi ni namba, uchaguzi ni takwimu," alisema Peter.

Aliwataka wananchi na wanachama wa chama hicho kutembea kifua mbele na kueleza mafanikio ambayo yamefanyika katika maeneo yao.

"Jambo jingine la kumpa zawadi Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa sababu mambo ambayo ametutendea ni makubwa sana kwenye kata yetu, Lazima sisi wanaCCM tuyasemee mafanikio haya yaliyotekelezwa na serikali ya awamu ya sita," alisema. Baadhi ya wakazi wa kata hiyo, akiwamo Clementina Mkinga, alisema kujiandikisha ni jambo muhimu kwa sababu ndiyo fursa pekee itayompa mwananchi fursa ya kupiga kura.

Mkazi huyo alitoa rai hasa kwa vijana kujitokeza na kugombea uenyekiti wa mtaa, kijiji na kitongoji katika uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika nchini mwezi ujao.



# Waziri awabana maofisa ustawi jamii kesi udhalilishaji kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

MAOFISA ustawi wa jamii wa mikoa na wilaya katika Kisiwa cha Pemba, wametakiwa kufuatilia kesi za udhalilishaji wa kijinsia na kuhakikisha zinafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Wito huo ulitolewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, wakati akizungumza na viongozi na maofisa hao kisiwani hapa.

Juma, alisema serikali imejipanga kuhakikisha kesi zinazofikishwa mbele ya vyombo vya sheria zinafanyiwa kazi na kushughulikiwa kwa haraka ili kutokomeza vitendo hivyo kisiwani hapa.

Alisema kumekuwa na malalamiko ya wananchi ikiwamo wazazi kutokana na tatizo la kuchelewa na kushughulikiwa kesi dhidi ya vitendo hivyo kwenye vyombo hivyo kuanzia Jeshi la Polisi hadi mahakama.

**Alisema kumekuwa na malalamiko ya wananchi ikiwamo wazazi kutokana na tatizo la kuchelewa na kushughulikiwa kesi dhidi ya vitendo hivyo kwenye...**

Hata hivyo, Waziri huyo alionyesha kufurahishwa na kasi ya mahakama kushughulikia kesi hizo na kutoa hukumu haraka.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Anna Athanas Paul, alisema wanafanya tathmini ya mwenendo wa kesi hizo ili kubaini ongezeko la matukio hayo.

Anna, alisema matukio ya kesi hizo, yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku licha ya kutolewa elimu jinsi ya kupambana nayo inayotolewa kupitia vyombo vya habari.

Ofisa Mwandamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Ahmed Rashid Ali, alisema wanatekeleza mradi wa jinsia ili kufahamu athari za matukio hayo na kukabiliana nayo.

Alisema elimu dhidi ya matukio hayo, shirika hilo litahakikisha inatolewa zaidi kuanzia ngazi ya shina hadi vijijini.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abulla, akikata utepe kuzindua Mfumo wa Taarifa za Elimu Shuleni (SIS), mjini Zanzibar juzi. Wengine ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa na Mkurugenzi Mkaazi wa USAID Tanzania, Craig Hart. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mfumo kuboresha utendaji sekta ya elimu Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imezindua mfumo wa taarifa za elimu kwa kutumia kompyuta lengo la kuboresha utendaji wa sekta ya elimu visiwani hapa.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alisema kuwa mfumo huo utaleta mabadiliko na kutatua changamoto ikiwamo kuchelewa utoaji maamuzi ya sera na utawala kwa wakati.

"Mfumo huu mpya utawezesha kazi za ukusanyaji, uchambuzi na matumizi ya takwimu kufanyika kwa urahisi, ufanisi mkubwa na kupunguza gharama," alisema Hemed.

Alisema serikali inakusudia ifikapo Januari mwakani shule ziendeshwe kwa mkondo mmoja.

Alisema kwa sasa asilimia 67 ya shule za msingi zinaendeshwa kwa mkondo mmoja na sekondari asilimia 86.

Alisema mfumo huo ni nguzo muhimu kuyafikia malengo ya mageuzi ya elimu nchini na kwamba serikali imewekeza fedha nyingi hasa katika sekta ya elimu. Hemed, alisema serikali pia imeweka malengo ya kufuta daraja sifuri katika ufaulu wa mitihani ya taifa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema serikali iwekeza mikakati ya kuboresha mifumo maalum ya kutoa taarifa ili kupata uelewa wa kuwafundisha na kufikia malengo ya ufaulu kwa wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari.

Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), Dk. Massoud Mohd Salim, alisema mfumo wa taarifa za elimu utasaidia kuimarisha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi.

Dk. Salim, alisema ili mfumo huo uweze kufanya kazi, kunahitajika ushirikiano kati ya wizara hiyo, walimu, wazazi na wadau wa elimu nchini kufikia mageuzi ya elimu Zanzibar.

Akiwasilisha taarifa ya mfumo huo, Naibu Katibu Mkuu Utwala wa Wizara ya Elimu, Khalid Wazir, alisema mfumo huo utasaidia ukaguzi, uandaaji wa mitihani na uchakataji wa taarifa za walimu na wanafunzi watoro ili kila mtoto apate haki yake ya msingi ya kusoma.

# Dk. Mwinyi, Gavana Comoro wateta

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema wakati umefika kurejesha diplomasia ya uchumi na kuendeleza biashara baina ya Zanzibar na ya Comoro ili kudumisha ushirikiano baina ya nchi hizo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar wakati akizungumza na Gavana wa Jiji la Moroni, Visiwa vya Ngazija, Ibrahim Mzee na ujumbe wake baada ya kuwasilisha nia ya kukuza ushirikiano baina nchi hizo.

Dk. Mwinyi, aliushauri ujumbe huo kurejesha makundi ya wafanyabiashara wa nchi hiyo kuja Zanzibar kuangalia fursa za biashara na uwekezaji kama ilivyokuwa miaka iliyopita.

Alisema ni vyema pande mbili hizo kufikiria namna ya kurejesha huduma ya usafiri wa vyombo vya baharini ili kuwanufaisha wananchi na fursa za biashara na jamii.

Mwinyi aliutaka ujumbe huo kuweka utaratibu maalumu kwa walimu wa Zanzibar kwenda Comoro kufundisha Kiswahili au wa nchi hiyo kuja visiwani Zanzibar kujifunza lugha hiyo kwa sababu zinashabihiana.

Gavana Mzee alisifu kasi ya mabadiliko na maendeleo ya Zanzibar na kusema nchi yake ina kitu cha kujifunza kama vilivyofanikiwa nchi hiyo.

Alitumia fursa hiyo, kumualika Mwinyi kuzuru visiwa vya Ngazija kwa lengo la kubadilishana uzoefu kwenye nyanja za maendeleo.

Eneo jingine aliloligusia ni kuimarisha ushirikiano wa karibu baina ya Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wakulima na Wenye Viwanda Zanzibar na Comoro ili kukuza biashara baina yao.

Akiambatana na ujumbe huo, Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Muhammed Mussa, alisema utakuwapo Zanzibar kwa siku tatu na kuwa na mazungumzo ya ushirikiano baina yao na Manispaa ya Jiji la Moroni.

Ujumbe huo utakuwa na siku maalum ya kutembelea Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao ni mji wa urithi unaotambulika na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa kwa lengo la kukuza ushirikiano.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SILVIA I. KANYOPA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0207/0125** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIRAENI GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/219636/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TIMA OMARI ZIMBWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0907-0035** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ZINGIBARI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/142661/2024**

**CHANGE OF NAME DEED POLL ACT (CAP 117**

**BY THIS DEED I ELISHA SIXTUS SALEO** ( new names) of P.O.BOX, ARUSHA DO HEREBY absolutely renounce and abandon the use of my former names **ELISHA SIXTUS KIKULA** (old name) in lieu thereof do assume the name **ELISHA SIXTUS SALEO** and in pursuance of such change of my names as aforesaid.

**I HEREBY DECLARE,** that I shall at all times hereafter and in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **ELISHA SIXTUS SALEO** as my name in lieu of **ELISHA SIXTUS KIKULA** the names I renounced as aforesaid.

**HEREBY AUTHORISE** ,and **REQUEST** all persons to designate and address me in the name of **ELISHA SIXTUS SALEO .**

**VERFICATION:**

**I , ELISHA SIXTUS SALEO** make this declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the provisions of the Oaths and Statutory Declarations Act,Cap . 117

**WITNESS WHEREOF I** have here unto subscribed the name ELISHA SIXTUS SALEO in on the day and in the manner hereinafter appearing.

SIGNED and DELIVERED by the said ELISHA SIXTUS SALEO who is known to me Personally/introduced to me by .................. the latter being known to me personally in my presence this 27 day of March , 2024

BEFORE ME:
NAME ....Patricia Remmy Lyimo....
SIGNATURE ..........
ADDRESS ....15018, DSM....
QUALIFICATION COMMISSIONER FOR OATHS



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAPTIST FELIX THILIA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA TOWNACE NOAH** yenye usajili namba **T 247 CCZ** na CHASSIS NAMBA: **SR500069235.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SOG/RB/4320/2024**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 25225 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ALOYCE GEORGE MKINI. DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**

1. **ESTHER JACOB FELISIAN. PETITIONER**
2. **____________________ PETITIONER**
3. **____________________ PETITIONER**

**GENERAL CITATION**

**(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 24 day of 10.2024

Dated at MOROGORO this 10 day of 10.2024

PRINCIPAL/ SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO DISTRICT COURT

## KUPOTEA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

**EZEKIEL JIMMY MASSANJA** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja **na 18 na 19 kitalu "MM"** kilichopo Lubaga Manispaa ya Shinyanga chenye jina la Massanja Chenge.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi
**PHQ/SHI/SHI/9617/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAMISI RASHID SHONGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye jina la umiliki **GS GROUP LIMITED** yenye usajili namba **MC 366 DYD** na CHASSIS NAMBA: **LC6PCJK22P0037728.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/RUV/SON/6714/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HEMEDI OMARI MWINSHEHE,** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari aina ya Vanguard yenye namba za usajili **T894DSF,** CHASSIS NAMBA **AGA385138838,** Engine No **2AZFE327380,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/45833/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JASSIM ALLY MUNGUTWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA STARLET** yenye usajili namba **T 869 ARS** na CHASSIS NAMBA: **JT152EP9100455026.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SOG/RB/4230/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HOSIANA JOHN MWAMBIIPILE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba **T 800 BVD .** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/SHI/KAH/6909/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 31/2024**

**MALISELA DESDERIUS SANGA.........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ZOOH MOHAMED KISALELE ..............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURI**

Mjibu maombi unataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa arthi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shauini bila kukosa au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 18/10/2024 saa 6:00 mchana. Shauri linakuja kwa ajili ya Uamuzi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusoma Uamuzi bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo name na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04/10/2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NICODEM FIDELIS LUPOGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 219 CKA** na CHASSIS NAMBA: **SR500046112.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SOG/RB/4020/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PHILMON SWEDY KILIMBE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 953 DEM** na CHASSIS NAMBA: **AZR600081891.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **SOG/RB/4220/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**( S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo ARUSHA MJINI**

**Usimamizi wa Mirthi 243 2024**

**Ombi la ZUKRA IDD B.MFINANGA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu IDD BAKARI MFINANGA WA**

**Kwa**
**YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 12/11/2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa Marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa .
Tarehe 08/10/2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ARUSHA

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA (LAND DIVISION) AT DAR ES SALAAM**
**MISC. LAND CASE APPLICATION NO. 119 OF 2018**
**KABULA AZARIA NG'ONDI & 3 OTHERS..... APPLICANTS**
**VERSUS**
**MARIA FRANCIS ZUMBA & ANOTHER .........RESPONDENTS**

**TO:**
**MSOLOPA INVESTMENT CO.LTD**
**P.O.BOX 40561**
**DAR ES SALAAM**

**NOTICE OF DATE FOR HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **HEARING ON 16th Day** of **OCTOBER 2024** at 1**0:00 PM** Before **HON. N.E.MANDAI, JUDGE.**
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without failure
**GIVEN UNDER MY** Hand and the Sea of the Court this 23rd day of **SEPTEMBER 2024**

DEPUTY REGISTRAR

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DAUD MATHIAS BWILINDE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye usajili namba **MC 727 DVB.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/SHI/KAH/8663/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BASHIRU MOHAMED MTACHILA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya TVS yenye usajili namba **MC 455 DDB.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/SHI/KAH/9599/2024**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**SUB- REGISTRY OF ARUSHA AT ARUSHA**

**TAXATION CAUSE NO. 21646 OF 2024**
**(High Court Civil Appeal No. 57 2023)**

**DAWID ANDRZEJ BRATKO......................DECREE HOLDER**

**VERSUS**

**TUMAINI MARK MANO.....................JUDGMENT DEBTOR**

**NOTICE OF MENTION**

**TO: TUMAINI MARK MANO**
**ARUSHA.**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High court at Arusha on 15th day of October, 2024 at 11:00hrs in the forenoon.
You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for mention, the court may proceed in your absence.

**VEN** under my **HAND** and **SEAL** of the **COURT** this **09th** day of **October, 2024**

A.H.Msumi
**DEPUTY REGISTRAR**
**ARUSHA**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ujenzi bandari ya uvuvi wafikia asilimia 70

**Na Mwandishi Wetu**

UJENZI wa bandari ya kwanza ya uvuvi ya Kilwa Masoko iliyoko kwenye pwani ya Bahari ya Hindi mkoani Lindi, uko karibu kukamilika, ikiwa tayari imefikia asilimia 70.

Mkurugenzi wa Miundombinu na Maendeleo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, George Kwandu, alisema jana kuwa mradi huo ni hatua muhimu katika mkakati wa Tanzania wa kukuza sekta ya uvuvi wa bahari kuu na kuboresha maisha ya wavuvi.

Alisema mradi huo ambao unagharimu Sh. bilioni 289.5, unatarajiwa kukamilika Januari, mwakani na kutengeneza ajira 30,000 huku ukiwa na uwezo wa kuchakata tani 60,000 za samaki kila mwaka.

Kwa mujibu wa Kwandu, moja ya vipengele muhimu vya mradi huo ni kituo cha kuchakata samaki ambacho kina lengo la kuwawezesha wavuvi wa ndani.

"Wavuvi watawezeshwa kuongeza mavuno yao kutoka kilo moja hadi kilo 100 kwa siku. Ongezeko hili litaongeza faida na kuboresha hali zao za kiuchumi," alisema.

Aidha, kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wanawake wanaoshiriki katika sekta hiyo wanatarajiwa kuona fursa zaidi katika kilimo cha mwani, huku uzalishaji ukitarajiwa kuongezeka kutoka tani 4,000 hadi 10,000 kwa mwaka.

Kwandu, alisema kwa sasa Tanzania haijafaidika kikamilifu na uvuvi wa bahari kuu kwa sababu sehemu kubwa ya samaki huvuliwa na meli kubwa za kigeni au kutupwa kwa kukosa vifaa vya usafirishaji.

"Bandari hii mpya itasaidia kutatua changamoto hizo, kuruhusu samaki ambao uvuaji wake hawajafungwa kwenye mikataba ya aina yoyote kuletwa Kilwa Masoko, ambapo watachakatwa na kuuzwa kwa wafanyabiashara, hivyo kuunda mnyororo wa usambazaji wenye ufanisi na faida zaidi.

„Bandari hii ya uvuvi italeta mabadiliko makubwa katika sekta ya uvuvi Tanzania. Itakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 1,800 za bidhaa za samaki kwa wakati mmoja na kuhudumia meli zenye urefu wa hadi mita 35,“ alisema.

Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko inatarajiwa kuwa kitovu cha uvuvi wa bahari kuu, ikileta miundombinu muhimu itakayokuza sekta ya uvuvi nchini Tanzania na kusaidia jamii za ndani kuongeza uzalishaji wao wa kiuchumi.

Mwezi uliopita, wakati wa Mkutano wa Nane wa Mawaziri wanaosimamia Bahari, Maji ya Ndani, na Uvuvi wa Shirika la Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki (OACPS), Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema wavuvi wadogo wanachangia kwa kiasi kikubwa sekta ya uvuvi nchini.

Ulega alisema asilimia 95 ya wavuvi wa Tanzania wanafanya kazi kwa kiwango kidogo, wakichangia kwa kiasi kikubwa uchumi na usalama wa chakula.

Tanzania huzalisha tani 472,579 za samaki kwa mwaka, huku tani 429,168 zikivuliwa kutoka kwenye maji ya asili. Sekta hiyo inachangia Sh. trilioni 3.4 kwa mwaka ikiwa na ukuaji wa asilimia 1.9 na kutoa ajira kwa za moja kwa moja 230,000.

Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko ni sehemu ya ajenda pana ya maendeleo inayolenga kuwawezesha wanaoshiriki katika sekta za uzalishaji wa Tanzania.

Wakati wa uzinduzi wa Bandari ya Kilwa Masoko, Rais Samia Suluhu Hassan pia alitaja mipango ya kujenga bandari nyingine kama hiyo Bagamoyo ili kufaidika na ukanda mpana wa pwani wa Tanzania.

Alisema Bandari ya Kilwa itafungua fursa sio tu kwa wavuvi, bali pia kwa wale wanaohusika katika mchakato wa kuongeza thamani, kama vile kilimo cha mwani na uchakataji wa samaki.



Umati wa wananchi waliofika kwenye kilele cha kambi ya upimaji wa macho bure iliyoendeshwa kwa siku mbili na Hospitali ya CCBRT katika Kituo cha kutolea huduma cha Kibo Complex Tegeta, Dar es Salaam jana, kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Afya ya Macho Duniani. Watu zaidi ya 400 walipatiwa huduma mbalimbali za upimaji macho na miwani. **PICHA: JOHN BADI**

# Pinda aeleza jitihada za Tanzania katika kukuza na kuendeleza miji

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ameeleza Tanzania inavyofanya jitihada kukuza na kuendeleza miji.

Pinda alisema hayo jana katika Kongamano la Kimataifa kuhusu Miji linalofanyika Vienna, Austria, akiongoza ujumbe wa Tanzania.

Kongamano hilo lililobeba kaulimbiu ya „Suluhu Bunifu kwa Miji ya Kesho" linafanyika kwenye Kituo cha Kimataifa cha Vienna, Austria kuanzia Oktoba 9 na kukamilika leo na kuhusisha viongozi na wataalamu wanaohusika na masuala ya usimamizi wa ukuaji na uendelezaji miji kutoka nchi mbalimbali.

Pinda alizitaja baadhi ya jitihada hizo kuwa ni pamoja na uamuzi wa serikali kuhamia Dodoma, matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwenye masuala ya ardhi, uanzishwaji Kituo cha Taifa cha Ubunifu na Mafunzo cha Taarifa za Kijiografia na maboresho mbalimbali ikiwamo ya Sera ya Taifa.

Naibu Waziri Pinda aliongeza kuwa kwa sasa Tanzania imeanza kutumia teknolojia ya kisasa kutambua wazalishaji taka ngumu ambayo imerahisisha namna ya kuwafikia watumiaji na ukusanyaji wa taka ngumu.

Kwa mujibu wa Pinda, jiji la Da es Salaam, tathmini inaonyesha kuwa teknolojia hiyo imekuwa ufanisi kwa asilimia 129 katika kutambua wazalishaji na maeneo taka ngumu yanapozalishwa kwa wingi ikilinganishwa na mfumo wa kawaida uliokuwa ukitumika kukusanya taka ngumu.

Kuhusu ushirikishwaji wananchi katika masuala ya uendelezaji miji, Pinda alisema Tanzania imebaini michango mikubwa ya wananchi katika upangaji na uendelezaji miji.

Alisema wananchi hushirikishwa kikamilifu huku akibainisha kuwa mfumo huo umeonekana kuleta tija katika upangaji na usimamizi wa miji na kutolea mfano katika Jiji la Arusha eneo la Mianzini ambako makundi mbalimbli ya jamii yalihusishwa na kushirikishwa katika kuandaa mpango wa uendelezaji wa eneo hilo.

"Wazee, vijana, kinamama na viongozi wa eneo husika walishirikishwa na sauti yao kusikika, huu nao ni ubunifu mzuri unaleta suluhu kwa miji ya kesho," alisema Pinda.

Pinda alilishukuru Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) kuandaa kongamano hilo muhimu lililowakutanisha viongozi wanaohusika na masuala ya usimamizi wa ukuaji na uendelezaji miji kushirikishana ubunifu na mbinu mpya ya uendelezaji wa miji ya kesho.

Lengo la kongamano hilo kujadili na kushirikishana juu ya suluhu bunifu kwa miji ya kesho na kutoa fursa kwa nchi wanachama kubadilishana uzoefu kwa mustakabali endelevu wa miji kwa watu wote duniani.

## Wapatiwa mafunzo ya kukabili udumavu

**Na Jenifer Gilla**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Kondo, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wamepatiwa wafunzo ya kilimo cha kisasa cha mboga na matunda kinachohimili athari za mabadiliko ya tabianchi ili kukabiliana na udumavu.

Mafunzo hayo yemetolewa ikiwa wiki moja tangu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi, kusema zaidi ya watoto milioni tatu nchini wana tatizo la udumavu, hali aliyosema ni mbaya kwa taifa la baadaye.

Akifungua mafunzo hayo mwanzoni mwa wiki, Msajili Msaidizi Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka Manispaa ya Kinondoni, Duraha Lipangu, alisema wanafunzi walijifunza kwa vitendo kwa kupanda miche ya matunda na mboga katika eneo la shule ambayo ikikua itakuwa na manufaa kwao.

Lipangu alisema hali hiyo itasaidia kupambana na magonjwa yasababishwayo na lishe duni kama vile utapiamlo na udumavu kwa kuwa wanafunzi hao watapata lishe kamili wakiwa shuleni.

"Mboga hizi zikikua tutaokoa wanafunzi wa shule hii na magonjwa yatokanayo na lishe duni kwa sababu watapata lishe bora wakiwa shuleni, hata wasipopata nyumbani," alisema.

Ofisa Kilimo kutoka Kituo cha Kilimo Malolo, Hamza Mkoka, alisema waliwafundisha wanafunzi hao namna ya kupanda mboga na miti ya matunda ndani kwa kutumia mifuko iliyotumika.

Pia alisema waliwafundisha kutumia mbolea na dawa za kuua vijidudu za kienyeji siziso na madhara kwa afya ya mwanadamu kama vile majani ya mwarobaini, aloevera na pilipili.

Alisema kilimo hicho kinafaa zaidi maeneo ya mjini kwa sababu hakihitaji eneo kubwa kwa kuwa yanapandwa kwenye ardhi moja kwa moja, pia kinatunza mazingira kwa sababu kinatumia vifaa vilivyokwisha tumika kama vile viroba, mifuko ya saruji na vyombo.

"Kwa hiyo baada ya kupata mafunzo haya, mitazamo ya wanafunzi hawa itabadilika. Badala ya kuona mifuko na vyombo vya plastiki vilivyochakaa kuwa ni taka, wataona ni mali ya kupandia mboga na matunda nyumbani kwao," alisema.

Ofisa Ufuatiliaji kutoka Youth Health Home Tanzania, iliyoratibu mafunzo hayo, Dennis Mango, alisema walishawishika kuanzisha programu hiyo baada ya kuona kuwa upatikanaji wa mboga na matunda mijini ni tatizo kutokana na uhaba wa maeneo.

Mchezaji wa ridhaa wa mchezo wa gofu, Asha Sugira, akipiga mpira kwenye mashindano ya Mkuu wa Majeshi 'CDF Golf Trophy 2024' yaliyomalizika hivi karibuni kwenye viwanja vya Lugalo. PICHA: MPIGA PICHA WETU



# USHINDANI WAONGEZEKA ZAIDI MASHINDANO YA GOFU YA CDF

**Na Faustine Feliciane**

SIKU tatu za mashindano ya gofu ya Mkuu wa Majeshi ‚NMB CDF Trophy' yaliyohusisha wachezaji zaidi ya 250, kutoka klabu mbalimbali za gofu Tanzania, yalihitimishwa Oktoba 6, 2024 huku kukiwa na ushindani mkubwa.

Mashindano hayo yalichezwa kwa siku tatu mfululizo kuanzia Oktoba 4 mpaka 6 mwaka huu katika Klabu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, JWTZ Lugalo Golf jijini Dar es salaam.

Wachezaji kutoka Klabu za Kili Golf, Arusha Gymkhana, Moshi Gymkhana, TPC Club, Morogoro Gymkhana, Kilombero Club, Mufindi Club, Dare es Salaam Gymkhana na wenyeji Lugalo, walishindana huku mshindi wa jumla akiondoka na kitita cha shilingi milioni 4 kama zawadi kutoka kwa wadhamini, Benki ya NMB, huku mwaka huu mashindano hayo yakienda sambamba na kudhimisha miaka 60 ya JWTZ.

Akizungumza wakati wa sherehe za kufunga mashindano hayo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Tanzania, Jenerali John Mkunda ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema, mashindano hayo yamezidi kupata umaarufu na kuongeza ushindani.

„Naushukuru na kuupongeza uongozi wa Lugalo Golf Club kwa kunialika kuja kufunga mashindano haya, niwapongeze pia kwa kuyaandaa mashindano haya.

Mashindano haya kwa mwaka huu yamekuwa sehemu ya kusherehekea miaka 60 ya Jeshi la Wananchi Tanzania tangu kuanzishwa kwake Septemba Mosi 1964.

Nichukue nafasi hii kumshukuru mwasisi wa mashindano haya Mkuu wa Majeshi mstaafu Jenerali George Waitara. Mchezo wa gofu haukuwa maarufu sana hapa nchini kama ilivyo michezo mingine lakini yeye aliangalia mbali kwa kuanzisha mashindano haya," alisema Jenerali Mkunda.

Alisema mashindano hayo yamekuwa na ushindani mkubwa kutoka kwa wachezaji mbalimbali huku akiainisha mafanikio ya klabu ya Lugalo ni kuona wanatengeneza wachezaji wa mchezo wa gofu ambao wana uwezo wa kuleta ushindani kimataifa.

„Mwaka huu timu yetu ya gofu ya Jeshi la Wananchi Tanzania ilishiriki mashindano ya mchezo wa gofu ya kimataifa huko Zimbabwe.

Katika mashindano hayo timu yetu ilipata matokeo ya kuridhisha, wanawake walishiriki walishika nafasi ya tatu na wanaume nafasi ya nane.

**Kwenye kutambua wachezaji wetu katika kushiriki michezo hiyo, Jeshi limeamua kuwazawadia wachezaji watatu wa kike waliofanya vizuri zaidi kuliko wenzao na kutuletea medali ya shaba. Ikumbukwe medali ya shaba ni miongoni mwa medali tatu zinazotambulika kimataifa," alisema na kuongeza,**

"Mwisho kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru mdhamini mkuu wa mashindano haya ambaye ni Benki ya NMB kwani benki hii imekuwa ikishirikiana nasi katika matukio mengi na kwa pamoja tumeweza kufanikisha mambo mengi," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Mkuu wa Wateja na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema, benki hiyo imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na Klabu ya Gofu ya Lugalo kwa muda mrefu na wameendelea kuwa wadau wakubwa wa mashindano hayo kwa miaka saba."

"Tumekuwa tukihakikisha tunashirikiana kwa dhati na Klabu ya Gofu ya Lugalo kuandaa kitaalamu mashindano haya," alisema Mponzi.

Rais wa Chama cha Gofu cha Wanawake (TLGU), Queen Siraki, kwa upande wake alipongeza uwepo wa mashindano hayo huku akifurahishwa na watoto kukumbukwa.

"Ili kuuinua mchezo wa gofu hapa Tanzania, katika mashindano yoyote ya wakubwa ni vizuri pia watoto kushindanishwa, nimefurahishwa na hilo kuzingatiwa katika mashindano haya kwani kuwapa nafasi watoto kuonyesha uwezo wao inawajenga ili baadaye waje kuwa wachezaji wazuri Zaidi," Queen.

**WASHINDI**

Katika mashindano ya mwaka huu, mchezaji Enoshi Wanyeche, kutoka Klabu ya Lugalo, aliibuka mshindi wa jumla baada ya kushinda kwa mikwaju ya grosi 224. Nafasi ya pili ilichukuliwa na Isiaka Daudi aliyepata grosi 226, huku Marius Kajuna akipata grosi 230 akishika nafasi ya tatu, wote kutoka Klabu ya Lugalo.

Ally Isanzu kutoka Klabu ya TPC, alishika nafasi ya nne baada ya kupiga mikwaju ya grosi 231 akifuatiwa na Michael Masawe kutoka Lugalo aliyepata grosi 233.

Katika kundi la wachezaji wa kulipwa, mchezaji kutoka Klabu ya Arusha Gymkhana, Nuru Mollel, aliibuka mshindi baada ya kupata alama za jumla 149.

Mollel aliondoka na zawadi ya fedha shilingi 2,000,000.

Isaac Wanyeche kutoka Klabu ya Golf ya Kilimanjaro alimaliza katika nafasi ya pili kwa alama ya 150, akapata zawadi ya shilingi 1,000,000.

Uamuzi wa kuangalia alama za nyuma ulimpa nafasi ya pili, kwani alikuwa na alama sawa na Elisante Lembris (150), ambaye alimaliza katika nafasi ya tatu.

## ZISIKUPITE

### RONALDO AMTAKA DE BRUYNE

MSHAMBULIAJI wa Al-Nassr na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 39, anahimiza klabu hiyo ya Saudi Arabia kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne wakati mkataba wa mchezaji huyo wa miaka 33 na Manchester City utakapokamilika msimu ujao. ***(Mundo Deportivo)***

### MAN UNITED YAMTAKA ALONSO

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumteua kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso kuchukua nafasi ya Erik ten Hag na wako tayari kumsubiri hadi msimu wa joto kwa kiungo huyo wa zamani wa Liverpool. ***(Todofichajes)***

### TORRES AWINDWA UNITED

MLINZI wa Aston Villa, Pau Torres anawindwa na klabu ya Manchester United ambao wako tayari kutoa karibu pauni milioni 42 kwa mlinzi huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 27. ***(Fichajes)***

### SALAH, VAN DIJK WATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Saudi Pro League, Al-Ahli inataka kumsajili mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32, na mwenzake wa Liverpool, Virgil van Dijk mwenye miaka 33, wakati mikataba yao itakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Caught Offside)***

### LEWANDOWSKI KUONGEZA MMOJA

MSHAMBULIAJI wa Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 36, ana chaguo la kuongeza mkataba wake na Barcelona hadi msimu ujao wa majira ya joto ikiwa atafikia vigezo fulani. ***(Sport)***

### FATI KUTOLEWA KWA MKOPO TENA

BARCELONA inafikiria kumtoa kwa mkopo mwezi Januari mshambuliaji wa Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 21, ambaye alikuwa na Brighton msimu uliopita. ***(Sport)***

### NKETIAH AFUNGUKA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 25 amesema aliondoka Arsenal na kujiunga na Crystal Palace msimu wa majira ya joto ili kupata „fursa ya kuwa uwanjani na kuimarika". ***(Independent)***

### DIAZ KUONGEZA MKATABA

LIVERPOOL inatarajiwa kufanya mazungumzo na winga wa Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 27 kuhusu mpango wa kuongeza mkataba wake hadi mwaka 2027 kufuatia mwanzo wake mzuri wa msimu huu. ***(Football Insider)***

### LARSSON AWA LULU ULAYA

KLABU kadhaa zinamfuatilia winga wa Eintracht Frankfurt aliye na umri wa miaka 20 kutoka Sweden, Hugo Larsson. ***(Fabrizio Romano)***

### DIBLING ATAKIWA KUBAKI

KLABU ya Southampton inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling mwenye umri wa miaka 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionesha nia ya kutaka kumnunua. ***(GiveMeSport)***

### CONNOLLY KUTUA SUNDERLAND

KLABU ya Sunderland inatazamia kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly mwenye umri wa miaka 24, kutoka Hull City. ***(Sun)***

DON A SOKA MAG A ULAYA



# TEN HAG KAMA KAWA MANCHESTER UNITED

**●●●Licha ya kutokuwa na uhakika wa kibarua chake, kocha huyo anajiandaa...**

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag anajiandaa kama kawaida kwa mechi inayofuata ya Manchester United dhidi ya Brentford, chanzo kiliiambia ESPN, licha ya kutokuwa na uhakika juu ya mustakabali wake.

Kamati ya utendaji ya klabu hiyo, ikiwa ni pamoja na wamiliki wenza Sir Jim Ratcliffe na Joel Glazer, walikutana kwa zaidi ya saa sita katikati mwa London siku ya Jumanne huku shinikizo likiongezeka kwa Mholanzi huyo.

Matokeo ya mapema msimu huu yaliyoifanya United kushuka hadi nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, yalijadiliwa katika mkutano huo pamoja na mada nyingine kadhaa.

Lakini bila maagizo ya wazi yaliyopokelewa tangu wakati huo, Ten Hag anaendelea kufanya kazi kama kawaida kabla ya kuwakabili Brentford, Old Trafford Oktoba 19.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba, Ten Hag amekuwa akiwasiliana na wafanyakazi wake ambao wamebaki Manchester wakati wa mapumziko.

United wamefanya siri kile kilichoamuliwa kwenye mkutano huo wa faragha ambao pia ulihudhuriwa na Mkurugenzi Mtendaji Omar Berrada, Mkurugenzi wa michezo Dan Ashworth, Mkurugenzi wa ufundi, Jason Wilcox na Mkurugenzi wa Michezo wa Ineos, Sir Dave Brailsford.

Ten Hag yuko likizo na anatazamiwa kurejea Carrington mapema wiki ijayo kuendelea na maandalizi ya kukabiliana na kikosi cha Thomas Frank.

United wako kwenye mbio za michezo mitano bila kushinda katika mashindano yote na wameshinda mara mbili pekee kwenye ligi msimu huu.

Wakiwa na pointi nane pekee katika michezo yao saba ya kwanza ambayo imejumuisha vipigo vya 3-0 nyumbani kutoka kwa Liverpool na Tottenham, ni mwanzo wao mbaya zaidi kuwahi kutokea kwenye kampeni ya Ligi Kuu.

Ni Southampton pekee walio katika nafasi ya 19 ambao wamefunga mabao machache. Ten Hag aliita kazi ya United „mradi wa muda mrefu" kufuatia suluhu na Aston Villa Jumapili na anaamini anaendelea kuungwa mkono na watu muhimu.



# Szczesny: Siwezi kuacha kuvuta sigara

**BARCELONA, Hispania**

GOLIKIPA wa Poland, Wojciech Szczesny ambaye alibadilisha uamuzi wake wa kustaafu soka na kujiunga na Barcelona, hayupo tayari kubadili maisha yake binafsi, na hivyo ataendelea kuvuta sigara.

Baada ya Marc-Andre ter Stegen kupata jeraha la muda mrefu, Barcelona walimshawishi kipa huyo wa zamani wa Juventus kusajiliwa kama mchezaji huru.

Szczesny haamini kwamba anachofanya nje ya uwanja kinapaswa kuwa na athari kwa mtu yeyote.

„Kuna mambo ambayo sibadilishi katika maisha yangu binafsi na si jambo la mtu yeyote ni kivuta sigara. Ninaamini kwamba haiathiri ninachofanya uwanjani, nafanya kazi kwa bidii,“ alisema Szczesny akiiambia Mundo Deportivo.

„Sifanyi hivyo mbele ya watoto kwa sababu sitaki kuwa na ushawishi mbaya kwao.

„Wakati mwingine mtu atachukua picha nikiwa na sigara, hiyo ni juu yao, sio juu yangu.

„Ikiwa mtu anafikiria kwamba nitabadilisha jinsi nilivyo katika maisha yangu ya kibinafsi wanaweza kufikiria tena kwa sababu niko vile nilivyo. Nimekuwa hivi maisha yangu yote.“



# MASHABIKI WAMJIA JUU KLOPP

**DORTMUND, Ujerumani**

BAADA ya kocha wa zamani wa Liverpool, Jurgen Klopp, kutangazwa kuwa msimamizi mkuu wa shughuli za soka katika kampuni ya Red Bull ambayo inamiliki klabu za RB Leipzig ya Ujerumani, RB Salzburg ya Austria, Red Bull Bragantino ya Brazil na RB New York ya Marekani, mashabiki wa Borussia Dortmund wamemvaa kocha huyo na kumwita msaliti.

Mashabiki hao ambao wengi wanaonekana kutofurahishwa na kitendo cha Klopp kukubali ofa hiyo kutoka kampuni ya vinywaji ya Red Bull ya nchini Austria, wamevamia kurasa za mitandao ya kijamii ya kampuni hiyo na baadhi ya machapisho yanayohusu kutangazwa huko kwa Klopp na kushusha matusi.

Mashabiki hao wanamlaumu Klopp kwa ‚usaliti‘ wa kujiunga na kampuni ya wapinzani wao kwenye Bundesliga kwa kuhofia huenda uwepo wake kwenye kampuni hiyo kutadhoofisha maendeleo ya Borussia Dortmund ambayo aliifundisha kabla ya kutimkia Liverpool.

Klopp aliyedumu Dortmund kwa miaka saba, amesaini mkataba wa ‚muda mrefu‘ ambao kwa mujibu wa taarifa una nafasi ya kumruhusu kuwa kocha mkuu wa timu ya taifa ya Ujerumani ikiwa atataka.

Kabla ya kukubali ofa hiyo, Klopp amekuwa kwenye mapumziko baada ya kumaliza safari ya miaka 9 ya kuifundisha Liverpool mwisho wa msimu uliopita.

Kwa upande wa kampuni ya Red Bull inasema Klopp hatahusika katika shughuli za kila siku lakini atazishauri timu kuhusu falsafa, mkakati wa uhamisho na maendeleo ya ukufunzi.

Klopp, raia wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 57 ataanza jukumu hilo Januari mosi 2025.

# Haaland kutoadhibiwa na FA

**MANCHESTER, England**

ERLING Haaland hatakabiliwa na adhabu kwa kumtupia mpira Gabriel Magalhães baada ya bao la dakika za lala salama la Manchester City dhidi ya Arsenal, kwa mujibu wa ESPN.

Kamera zilimnasa Haaland akirusha mpira nyuma ya kichwa cha mlinzi wa Arsenal baada ya John Stones kufunga na kufanya ubao kusoma 2-2 kwenye Uwanja wa Etihad katika mchezo wa Ligi Kuu England.

Tukio hilo halikuonwa na mwamuzi wa uwanjani Michael Oliver, lakini lilionekana na mwamuzi msaidizi wa ‚video‘ John Brooks, ambaye aliamua kuwa haikuwa vurugu.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba FA inafurahi kwamba tukio hilo lilishughulikiwa wakati huo na Haaland hatakabiliwa na hatua za kinidhamu.

Haaland, ambaye alifunga na kuifanya City kuwa mbele kwa bao 1-0 mapema kwenye mchezo huo, alihusika katika majibizano makali na kocha wa Arsenal, Mikel Arteta na mshambuliaji Gabriel Jesus baada ya filimbi ya mwisho.

Wachezaji wa City walikasirishwa na kile walichokiona kuwa kupoteza muda na Arsenal walipojaribu kucheza kipindi cha pili wakiwa na wachezaji 10 baada ya Leandro Trossard kuoneshwa kadi nyekundu.

Kamera za Sky Sports pia zilirekodi Haaland akigombana na Jesus baada ya filimbi ya mwisho baada ya kumwambia Arteta „awe mnyenyekevu.“

„Kuwa mnyenyekevu, eh; kuwa mnyenyekevu, eh,“ mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alimwambia kocha wa Arsenal, ambaye hakujibu.

Wakati wa mabishano makali na Jesus, Haaland alimwita mshambuliaji huyo wa Arsenal mara mbili kama „mcheshi.“

HABARI MICHEZO

# PAMBA FC YAWEKA VIKAO KUJADILI VIPIGO LIGI BARA

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kufanya vibaya kwenye michezo yake saba ya mwanzo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, viongozi na benchi la ufundi la Pamba Jiji FC wamekuwa kwenye vikao kujadili mwenendo huo na kuangalia nini cha kufanya ili kujikwamua.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo yenye maskani yake jijini Mwanza, Moses William, alithibitisha kuwapo kwa vikao hivyo ambavyo amevitaja vimekuwa vyenye tija na manufaa kwa maslahi mapana ya klabu hiyo.

Pamba Jiji FC ambayo imepanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu huu, ndiyo timu pekee ambayo haijashinda mchezo wowote wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa kati ya mechi saba ilizocheza, ikiburuza mkia na pointi zake nne.

"Kimsingi kulikuwa na vikao vya hapa na pale kufanya tathmini ya mwenendo ya klabu baina ya benchi la ufundi na manejimenti.

Vikao hivyo vimekuwa na tija na vimekuwa na manufaa kimsingi na maslahi mapana na Pamba Jiji.

Haya matokeo tuliyoyapata yanatukumbusha kuwa sisi tupo wapi na tunatakiwa tufanye nini, imekuwa vizuri kwamba ni mapema kwa hiyo tunayo nafasi ya kusahihisha makosa, tuwaambie mashabiki wetu kwamba ni kweli tumeanza vibaya ila hatuna timu mbaya, ni ubora wa wapinzani wetu, kwani tumekutana na ratiba ngumu mwanzoni mwa ligi," alisema Ofisa Habari huyo.

Katika michezo yake saba iliyocheza, imetoka sare michezo minne na kupoteza mitatu, huku mchezo uliopita ilipokea kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Yanga, mchezo uliochezwa, Oktoba 3, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. Mbali na hilo, amesema tayari wachezaji wa timu hiyo wamesharejea mapumzikoni na kuanza mazoezi kujiandaa na mchezo utakaofuata dhidi ya Kagera Sugar, utakaochezwa Oktoba 21, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

"Nadhani baada ya vikao mambo yataenda kama tulivyotarajia, lakini pia baada ya ratiba ngumu ya kucheza na timu ya Singida Black Stars, Yanga, Prisons, Mashujaa, tutaanza kufanya vizuri," alisema.




Wasanii wa Kikundi cha Safi Theatre wakicheza ngoma ya asili wakati wa uzinduzi wa benki moja jijini, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Coastal yakimbilia Arusha

Na Mwandishi Wetu

HATIMAYE klabu ya Coastal Union imetangaza kuwa itautumia Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, kama uwanja wake wa nyumbani katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuanzia sasa.

Hii ni baada ya tetesi za muda mrefu kuwa viongozi wa timu hiyo wanataka kuipeleka timu hiyo jijini humo, badala ya Dar es Salaam, ambapo ilikuwa ikitumia viwanja vya KMC Complex na Azam Complex, kwa michezo ya nyumbani.

Coastal ilikuwa ikitumia viwanja hivyo kutokana na uwanja wake halisi, Mkwakwani uliopo Tanga kuwa katika matengenezo.

Taarifa iliyotowa jana na klabu hiyo ilisema wameamua kuzipeleka mechi zao jijini humo kutokana na sababu mbalimbali ambazo baadhi yake ni kuthamini mapendekezo ya wanachama na mashabiki wao na kuirudisha timu Kanda ya Kaskazini, pamoja na ombi la mashabiki wa soka wa Arusha.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Abbas El Sabri, amesema licha ya kuhamia Arusha, lakini watarejea uwanjani wakiwa na kocha mpya ambaye watamtangaza hivi karibuni.

"Tutatumia kipindi hiki cha kalenda ya FIFA kuendelea kukipa makali kikosi chetu kwani hatukuanza vizuri, lakini pia tutarudi upya tukiwa na nguvu, benchi letu likiwa limeimarishwa tukiwa na kocha mpya, kwa sasa tunamaliza mazungumzo ya mwisho na mwalimu tunayemhitaji na ni mmoja wa makocha bora kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki," alisema Sabri.

Alisema kocha huyo alikuwa sehemu ya waliohudhuria mchezo kati ya timu yao dhidi ya Simba uliochezwa Ijumaa iliyopita, Uwanja wa KMC, Mwenge, uloisha kwa sare ya mabao 2-2.

"Kwa sasa yupo Tanga tunamalizia mazungumzo kabla ya kumtangaza, tumeshampa malengo yetu na ameyakubali," alisema.

Kwa sasa nafasi ya Kocha Mkuu kwenye kikosi hicho kinakaimiwa na beki wa kushoto wa zamani wa timu hiyo miaka ya 1980, Joseph Lazaro.

Timu hiyo inashika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu yenye timu 16, imekusanya tano pekee.

## Mkude: Simba SC, Yanga zinafanana

INATOKA UK. 24

"Mimi mchezaji aliyenishangaza sana nilipomwona kwa mara ya kwanza mazoezini kutokana na uwezo wake ni Joshua Mutale, na kambini kwetu kama asipokuwepo kila mtu anajua hayupo kwa sababu ni mwongeaji sana, humu kambini mchezaji ambaye ni mchekeshaji sana ni Kelvin Kijili na Ali Salim yeye huwa anawahi sana kwenye chakula," Kagoma alisema.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkude ambaye alijiunga na Yanga msimu uliopita akitokea Simba, alisema alichogundua timu hizi mbili zinafanana na mambo mengi ikiwa ni pamoja na aina ya maisha na mazingira ya kambi huku mashabiki wao wanazifanya ziwe klabu zenye ushawishi mkubwa.

"Mimi siyo mchezaji wa kwanza kutoka Simba kuja Yanga, vile vile kuna wachezaji ambao wametoka Yanga kwenda Simba, ukikaa nao watakwambia hivi hivi, ni majina tu ndiyo yanabadilisha, hizi ni timu kubwa ambazo aina yao ya kambi, usafiri, benchi la ufundi na uongozi vinafanana na kwa bahati nzuri mimi sijacheza timu nyingine zaidi ya hizi mbili," alisema Mkude ambaye ni zao la kikosi cha pili cha Simba.

Kiungo huyo ambaye alikuwa na uhakika wa namba katika kikosi cha kwanza cha Wekundu wa Msimbazi alisema timu hizo mbili zinabebwa na mtaji mkubwa wa mashabiki, bila wao ni kama hakuna kitu.

„Mashabiki ndiyo watu wanaweza kufanya mpira kuwa rahisi kwenye timu, ukiangalia mashabiki wa Yanga wamekuwa ni watu wenye sapoti kubwa sana na timu yao, na hata mashabiki wa Simba kwa upande wao ni watu ambao wanapenda timu yao, yaani hizi timu mbili bila mashabiki hakuna kitu," alisema Mkude.

Kuhusu mchezo wa dabi utakaochezwa Oktoba 19, mwaka huu, Mkude alisema hajawahi kuwa na presha katika mchezo wowote unaozikutanisha timu hizo.

Aliongeza kama akipata nafasi basi mashabiki wataona kitu ambacho atafanya, kwa sababu yeye ndiyo atakuwa mmoja wa wachezaji watakaocheza dabi nyingi zaidi pamoja na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' pamoja na Shomari Kapombe.

"Tunaendelea na mazoezi, dabi ni mechi ya kawaida kama nyingine, tatizo linakuja tu pale majina ya timu zinazocheza ni Simba na Yanga, labda hii ni kwangu kwa sababu nimeshacheza sana mechi hizi, binafsi sina presha, hata nikiamshwa usingizini naenda kucheza," aliongeza kiungo huyo. Mkude ambaye alipandishwa kutoka katika kikosi cha U-20 na kuanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2011/2012, alitaja mchezo wake anaoukumbuka zaidi akiwa Simba ni ule ya raundi ya pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, dhidi ya Nkana Red Devils ya Zambia, Simba iliposhinda mabao 3-1 na kufuzu hatua ya makundi baada ya miaka mingi kupita.

Amemtaja nyota aliyekuwa anamhusudu na kuiga ubora wake ambao umechangia kufika hapo alipo ni kiungo wa zamani wa Simba, Mwinyi Kazimoto huku kwa sasa anavutiwa na Kelvin Nashon, ambaye anaichezea, Singida Black Stars.

Michezo
Ijumaa Oktoba 11, 2024
Nipashe

Ten Hag kama kawa Man United
UKURASA 21





# Mkude: Simba, Yanga zinafanana

## ●●● Fadlu abadili 'gia' Msimbazi, nyota wafunguka ‚uteja' basi...

Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize akipambana kumiliki mpira katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC iliyochezwa hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amebadili aina ya mazoezi katika kikosi chake kuelekea mechi ya watani wa jadi, kiungo mkabaji wa Yanga, Jonas Mkude, amesema mazingira na maisha katika klabu mbili kongwe nchini, yanafanana.

Simba na Yanga zinatarajia kukutana katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara Oktoba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wakizungumza jijini wachezaji wa Simba, Edwin Balua, Mzamiru Yassin na Yusuph Kagoma, wamesema wamekuwa katika maandalizi ‚makali' ya kujiandaa na mchezo huo kwa sababu wamechoshwa na ‚uteja'.

Balua aliliambia gazeti hili kocha wao Fadlu, pamoja na benchi la ufundi, wamewabadilishia aina ya mazoezi kwa sababu wanahitaji kuona wameimarika huku akikiri mechi hiyo haitakuwa nyepesi.

"Hautakuwa mchezo mwepesi kwa sababu ni dabi, tumejiandaa vizuri, kama sisi wachezaji tumeanza maandalizi makali kuelekea kwenye mchezo huo. Kuna maandalizi ya tofauti kabisa, programu zimebadilika na hii inahusiana na mchezo huo, ila kwetu sisi hakuna kitu ambacho ni kigeni kwenye aina ya mazoezi hayo," alisema winga huyo aliyesajiliwa dirisha dogo msimu uliopita akitokea Tanzania Prisons.

Mzamiru kwa upande wake alisema hakuna dabi ambayo ni rahisi, lakini kwa upande wao wamejiandaa si kushinda mechi hiyo tu, bali kutwaa ubingwa msimu huu kwa sababu wamechoshwa na uteja wa misimu mitatu mfululizo.

"Kwa msimu huu tumejiandaa na vitu vingi, kuwafunga Yanga na ubingwa, ni msimu wa tatu hatupati chochote, sisi kama wachezaji tumechoshwa na uteja, ndiyo maana unaona msimu huu maandalizi yamekuwa makubwa mno," alisema Mzamiru.

Naye Kagoma, aliyesajiliwa msimu huu akitokea Fountain Gate, amesema ameshangazwa na mazingira aliyoyakuta kwenye klabu yake mpya ambapo ni tofauti na alipotoka.

Kagome ameeleza kufurahishwa na mazingira ya kambi, pamoja na ushirikiano mzuri anaopata kutoka kwa wachezaji wenzake.

INAENDELEA UK. 23

# Kufuzu AFCON 2025 kwetu ni deni - Stars

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI jana usiku ilishuka kuvaana na wenyeji DR Congo katika mechi ya Kundi H, Nahodha Msaidizi wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr', amesema wachezaji wanafahamu wana ‚deni' la kupambana kuhakikisha wanapata tiketi ya kushiriki Fainali zijazo za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2025).

Taifa Stars itarudiana na DR Congo Oktoba 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza kabla ya kushuka dimbani jana, Zimbwe Jr, alisema kila mchezaji ambaye yuko katika kikosi hicho anajua kiu ya Watanzania ni kuona wanapata tiketi ya kushiriki fainali hizo za Afrika.

Beki huyo alisema ushirikiano wanaopata kutoka kwa serikali na wadau wa soka nchini, unawaongezea nguvu ya kupambana na kuhakikisha wanafikia malengo.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morocco, alisema kikosi chake kinaendelea kuimarika na watacheza mechi zote, wanacheza bila presha yoyote.

Morocco alisema wanamheshimu kila mpinzani wanayekutana naye na wanajua kila timu inaposhuka uwanjani ina malengo ya kuondoka na pointi tatu.

"Tunaendelea kuimarika kadri tunavyoendelea kucheza mechi, tunapokuwa nje hatuna presha, tunapigana kuhakikisha tunapata matokeo, na nyumbani tunacheza bila presha. Watanzania waendelee kutusapoti, wana kiu ya kuona timu yao inafanya vizuri.

"Kwa niaba ya wachezaji tunamshukuru Mama yetu Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa mdau mkubwa, Mtanzania namba moja, ni kitu cha faraja, ametupa ndege, amefanya mengi, na sisi kwa nafasi yetu tunatakia kusaka ushindi," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042